# Nipashe

Ijumaa Julai 17, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580286

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO

"Kaa umbali wa mita mbili unapokuwa kwenye mikusanyiko."

2 mtr

USICHUKULIE POA

UNATEGEMEWA


**Wachambuzi watoa siri wanawake CHADEMA kung'ara kura za maoni**



UKURASA 2

# JPM awakana watia nia wa ubunge CCM

• **Asema** hakuna hata mmoja aliyemtuma, ataka wote watendewe haki, Samia aonya 'walafi' wa madaraka... *Endelea ukurasa 2 & 3*



Aliyekuwa kada wa CCM, Bernard Membe, akisalimia wanachama wa ACT-Wazalendo, kabla ya kutangaza rasmi kujiunga na chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo Taifa, Seif Sharif Hamad (kushoto), Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Mkoa wa Dar es Salaam, Salum Soud. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Sura mpya zaendelea kuchomoza majimboni

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Membe atua rasmi ACT- Wazalendo

UK. 2


MICHEZO YANGA BADO YAWEWESEKA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## Siri wanawake CHADEMA kung'ara zatajwa

**Na Salome Kitomari**

WANAHARAKATI mbalimbali wameanika siri ya wanawake ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kung'ara katika kura za maoni za kuwania ubunge kuwa ni ujasiri na uthubutu na kwamba hatua hiyo ni ya kupongezwa.

CHADEMA inaendelea na kura za maoni kwenye majimbo na hadi sasa ni katika majimbo 22 tu ambayo wamewashinda wanaume waliojitokeza.

Mchambuzi na Mtetezi wa Haki za Wanawake, Dk. Ananilea Nkya, alisema wanawake walioshinda katika majimbo hayo ni ambao wakiwa bungeni waliisimamia serikali, kuuliza maswali na kwenda majimboni kutoa mrejesho jambo ambalo liliwapa nafasi ya kuaminika kwa wananchi.

Nkya ambaye alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Wahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) mwaka 2001 hadi 2012, alisema wanawake wana sifa ya uaminifu na uongozi bora na wamethibitisha katika uongozi wenye matokeo kwa walioingia kwa lengo la kusaidia jamii.

"Katika vyama vya upinzani, mfumo wa kujenga watu wanaoingia kuwa viongozi unawajenga wanawake kuwa majasiri zaidi. Kwa asili wanawake ni majasiri, wanalea watoto na waume zao. Anapopata fursa kwenda kwenye siasa anakuwa majasiri zaidi," alisema. Dk. Nkya alisema siasa za upinzani ni ngumu na wanawake wameingia huko kutokana na kujengewa ujasiri na kwamba maisha ya wanawake tangu wakiwa wadogo ni kutafuta kuni na kuchota maji, hivyo wana ujasiri wa toka wakiwa wadogo kwamba wanapewa majukumu na uvumilivu,

"Ukiangalia wanawake wengi wa vyama vya upinzani hasa CHADEMA wengi waliopita, ambao walikuwa viti maalum na unaona pilikapilika walizopitia ikiwamo kufungwa na kushtakiwa," alisema.

Naye Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe, alisema ni hatua nzuri kwa kutoa nafasi kwa wanawake kuongoza majimbo na kwamba kinachotakiwa ni ulingo uwe sawa ili wapatikane viongozi bora, viongozi aliopata nafasi ahakikishe anajiandaa vizuri kuandaa sera za vyama vyao.

# JPM awakana watia nia ubunge CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amesema hajamtuma mtu yeyote kuwania uongozi na wanaodai kuwa amewatuma kuwania nafasi katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni waongo.

Alitoa kauli hiyo jana kwenye viwanja vya Ikulu, Chamwino jijini Dodoma wakati wa hafla ya kuapishwa kwa viongozi walioteuliwa hivi karibuni, wakiwamo wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na wilaya na Mkurugenzi Mkuu wa TIC, Dk. Maduhu Kazi.

Alisema kuna mtu yeyote anazungumza kuwa yeye amemtuma kwenda kugombea, ni muongo na ujumbe huo uwafikie wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuwataka kuwapima wagombea kwa jinsi wanavyowaona na watakavyofaa kuwawakilisha.

"Niwaombe tu wakazingatie nidhamu na maadili ya chama chetu na ninataka kuwathibitishia wananchi na wanaCCM, hakuna mtu yeyote aliyetumwa na mimi, hakuna mtu yeyote aliyetumwa na Makamu wa Rais, hakuna mtu yeyote aliyetumwa na Waziri Mkuu, hakuna mtu yeyote aliyetumwa na Mzee Mangula, hakuna mtu yeyote aliyetumwa na Katibu Mkuu, Dk. Bashiru," alisisitiza.

"Siwezi kumtuma mtu kupitia mgongo wa pembeni, wote wapo sawa, wapimeni kisawasawa kwa sababu nimesikia kila mahali 'mimi nimetumwa na Rais'. Sasa, kama ningekuwa na uwezo wa kutuma, mimi nihangaike kukutuma, si ningesubiri viti vyangu 10 nikakuteua kama nitashinda. Kwa hiyo, sikutuma mtu na ninajua Watanzania mnaelewa.

"Ukienda huko ukatumwe na wala hawakutumwa na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, asije mtu akasema ametumwa na IGP au CDF, angekutuma si angekuteua hata kanali."

Rais Magufuli pia aligusia mwitikio mkubwa wa makada wa CCM kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya chama kukiwakilisha katika kuwania nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani, akibainisha kuwa hadi jana asubuhi, waliokuwa wametangaza nia walikuwa zaidi ya 8,000, Mkoa wa Dar es Salaam ukiongoza.

"Dar es Salaam hadi leo (jana) alfajiri wapo 829, Arusha 320 na mikoa mingine, Kusini Unguja wapo 53, Kilimanjaro 82, Kagera 328, na hivyo kuwafanya watia nia kwenye majimbo kupitia CCM kuwa 6,533, lakini wanaopitia ubunge viti maalum 1,539 na kupitia wawakilishi 133 na hivyo jumla ni 8,205," alibainisha.

Alisema kujitokeza huko kwa watia nia kunadhihirisha kwamba CCM inapendwa na watu na kuwapongeza wale wote waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali. Rais Magufuli aliwataka wateuliwa, kwenda kufanya kazi na kuvumilia kwenye maeneo yao huku wakimtanguliza Mungu.

"Nipende kusisitiza kwamba katika kazi hizi kuridhika ni kitu muhimu sana, yule kijana pale anaitwa Suleiman ni 'PhD holder', lakini alikuwa anapata mshahara wa Sh. 500,000.

"Amefanya kazi yake makao makuu ya CCM na aliridhika kwa sababu kazi yake ilikuwa ni utumishi, aliridhika na mshahara wa Sh. 500,000. Ilipojitokeza fursa ndiyo tukamteua Mkuu wa Wilaya ya Kongwa," alisema.

"Sifahamu wakati mwingine vijana hawaridhiki, hasa waliozaliwa miaka ya 82, lakini ni matumaini yangu ataenda kuitumikia kazi yake vizuri, mmefanikiwa kupata nafasi kwa sababu mnaweza, nina uhakika mtaenda kusaidia taifa hili.

"Aliyekuwa RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) Dar es Salaam umefanya kazi sehemu nyingi na leo (jana) umekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ndugu Kirigini Joseph nina fahamu umekuwa Mkuu wa Mkoa ni mchumi mzuri, umefanya Jimbo la Ruangwa baadaye ukaenda Hanang' leo unaenda Manyara," alisema.



Rais John Magufuli akimwapisha, Aboubakar Kunenge kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Membe atua rasmi ACT- Wazalendo

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, amejiunga rasmi na Chama cha ACT-Wazalendo, huku akisema hatafuata nyayo za makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliohamia upinzani kisha kurejea katika chama hicho tawala.

Membe alitoa ahadi hiyo jana jijini Dar es Salaam, baada ya kupokewa rasmi na chama hicho.

Mwanasiasa huyo alijiunga na chama hicho Julai 8, mwaka huu, baada ya kufukuzwa na CCM Februari 28 kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo kukiuka kanuni na miongozo ya chama.

Membe ambaye ni mwanadiplomasia mbobezi, alisema hatakuwa kama wale waliojiunga na upinzani na baadaye wakarudi tena CCM.

Licha ya kuwa hakuwataja majina, wanachama waliohamia upinzani kutoka CCM na baadaye kurejea CCM ni waliokuwa mawaziri wakuu katika serikali za awamu ya tatu na ya nne, Frederick Sumaye na Edward Lowassa.

Vigogo hao walijiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Lowassa kupewa nafasi ya kugombea urais kupitia uliokuwa muungano wa vyama vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA). Vyama hivyo, mbali na CHADEMA, ni NCCR- Mageuzi, Chama cha Wananchi (CUF), National League for Democracy (NLD).

ATOA SOMO UPINZANI

Membe pia alisema kama vyama vya upinzani vitaweka ubinafsi pembeni na kushirikiana katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, milango ya kuingia Ikulu iko wazi.

Aliiomba kambi rasmi ya upinzani nchini ambayo ni CHADEMA, kukubali kuungana ili kuiondoa serikali iliyoko madarakani inayoundwa chama tawala.

"Kwa vyama vyote vikubwa na vidogo tuwaige wenzetu wa Malawi (vyama vya upinzani viliungana na kushinda uchaguzi). Tuache ubinafsi pembeni tuache tamaa zingine pembeni.

"Tuungane katika ngazi ya taifa, twende kifua mbele kuchukua uongozi wa nchi ambao barabara iko wazi. Nina imani na viongozi wa ACT-Wazalendo watalibeba hili," alisema Membe.

Huku akishangiliwa, Membe alisema hakuna kipindi ambacho milango ya Ikulu iko wazi kama ilivyo sasa hivi.

"Upinzani kuwa na mgombea mmoja milango ya Ikulu iko wazi kuliko tangu tulipopata uhuru (Desemba 9, 1961)," alisisitiza Membe huku akitoa rai kwa kambi ya upinzani kuungana ili kuitoa serikali iliyoko madarakani inayoundwa na CCM.

Katika mkutano huo, barua iliyoandikwa na Membe ilisomwa naa Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad. Membe aliandika barua hiyo Julai 8, mwaka huu, kwenda kwa Maalim Seif, kuitikia ombi la wanachama na viongozi wa ACT-Wazalendo la kumtaka kujiunga nao.

Miongoni mwa viongozi waliompokea Membe jana ni Maalim Seif Sharrif Hamad, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, Makamu Mwenyeviti wa chama hicho, Juma Duni Haji (Zanzibar) na Doroth Semu wa Bara.

# Magufuli akemea TIC danadana wawekezaji

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli amekemea tabia ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kuwapiga danadana wawekezaji kiasi cha kuwakatisha tamaa, jambo linalochangia kuikosesha nchi mapato na ajira.

Alitoa onyo hilo jana kwenye viwanja vya Ikulu, Chamwino jijini Dodoma wakati wa hafla ya kuapishwa kwa viongozi walioteuliwa hivi karibuni, wakiwamo wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na wilaya na Mkurugenzi Mkuu wa TIC, Dk. Maduhu Kazi.

"Kwa Mkurugenzi wa TIC, kahakikishe tunapata wawekezaji wengi. Pamekuwa na tabia ya wawekezaji wengi kuanza kuzungushwa, mwekezaji amekuja na hela yake, wewe kwanini umzungushe?" Rais alihoji.

"Tusiwazungushe wawekezaji. Tunahitaji wawekezaji hiyo ni fursa, ukishakuwa na wawekezaji, wakajenga kiwanda, tutatengeneza ajira na kukusanya mapato.

"Lakini, kumekuwa na njoo hapa, fanya hiki na hiki. Sasa nikuombe Daktari, kahakikishe mwekezaji hata akija leo (jana) anachokitafuta apate, hata maeneo ya uwekezaji apewe," aliagiza.

Rais Magufuli alisema ardhi kwa ajili ya kujenga viwanda ipo kila mkoa, akitolea mfano eneo la Kigamboni ambako kuna hekta zaidi ya 100 ambazo zililipiwa zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda pamoja na eneo la Kibaha ambayo yote hayajatumika.

"Kavutieni wawekezaji waje wawekeze, tusiwazungushe. Kuna mwekezaji kutoka Misri anataka kujenga kiwanda cha vifaa vya umeme, ninasikia amezungushwa kweli, kayasimamie haya ambayo, nina imani utayasimamia vizuri.

"Kila mmoja katika eneo lake akafanye anayoona yanafaa na siyo kwamba tumekuwa tukifanya hivi (mazoea), bali iwe tunafaya hivi, ninataka kila mteuliwa alishughulikie," aliagiza.



Katibu wa UVCCM Wilaya ya Kinondoni, Ally Simba (kulia), akimkabidhi fomu ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa kugombea ubunge Jimbo la Kinondoni, Iddi Azzan, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia aonya walafi wa madaraka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewataka viongozi wanaoteuliwa, kutosheka na nafasi zao badala ya kuhaha na madaraka.

Alitoa onyo hilo jana Ikulu Chamwino mkoani Dodoma wakati wa hafla ya kuapishwa kwa viongozi mbalimbali walioteuliwa juzi na Rais John Magufuli, akisema utawala wa sasa nchini unataka utumishi wa watu na si kuhaha na madaraka.

"Hongereni sana katika nafasi na ngazi tofauti mlizoteuliwa. La kuwaambia ni kwamba utawala wetu Tanzania sasa hivi ni utumishi, ni utawala wa utumishi wa watu na si utawala wa kuhaha na madaraka.

"Na imempendeza Rais kuwamegea wale wakuu wa mikoa na wilaya sehemu ya himaya yake. Mkakae na kuzitawala na kuwatumikia watu siyo kuziongoza bali kuwatumikia watu.

"Mnapokwenda wengine mmetoka kwenye maeneo hayo hayo. Kwa hiyo, mnajua mazuri na mabaya yapo wapi na jinsi ya kurekebisha. Kwa wale wapya, nendeni someni, mnaweza kurekebisha na mnavyorekebisha ndiyo maendeleo na mnavyorekebisha ndiyo tunasonga mbele, niwaombee kila la heri mkatumikie watu," alisema.

Makamu wa Rais alisema kuna haja viongozi kutosheka na nafasi walizonazo badala ya kutaka kupata kina nafasi ya uongozi inayojitokeza.

"Nadhani mtajifunza na somo, mwanadamu unapoishi lazima utosheke na kile ulichonacho na unapokuwa hutosheki, unahaha huku na huku, aaah sijui Mungu naye atakufungulia njia ipi unayoitaka. Kama ni kulia au kushoto Mungu ndio anajua maamuzi yake, kaeni, fanyeni kazi, tumikieni wananchi," alisema.

Katika hafla hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, aliwataka wateuliwa hao kwenda kufanya kazi na si kutafuta umaarufu.

"Niwapongeze nyie wote ambao Rais amewapima na kuwapa dhamana. Mimi nina hakika kwamba katika walio bora, ninyi ni bora zaidi na mtamsaidia Rais katika maeneo mbalimbali. Niwaombe sana msiende kutafuta umaarufu, kafanyeni kazi umaarufu uwatafute ninyi," aliagiza.

Jafo alisema wanaotafuta umaarufu mara nyingi mafanikio huwa si mazuri, lakini wakifanya kazi kama ambavyo Rais alivyowapa dhamana, anaamini umaarufu utawatafuta badala ya kuutafuta.

"Kwa wale ambao tutafanya kazi chini ya mamlaka ya serikali za mitaa, huku tumebadili utendaji kazi, huku sasa watu wanafanya kazi. Nendeni mkahakikishe fedha zilizopelekwa huko mnazisimamia. Huwa haipendezi unatoka hapa, unafika 'site' (eneo la mradi) jukumu ambalo alipaswa kufanya mkuu wa wilaya, unakuta halijafanyika vizuri," alisema.

Aliwataka kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha, akibainisha kuwa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2014/15, ilionyesha mamlaka hizo zilipata hati safi kwa asilimia 29, lakini sasa zimefikia asilimia 95.

"Hii inaonyesha tangu Rais Magufuli alipoingia, usimamizi wa fedha umeimarika. Ni jukumu letu kuhakikisha mnafanya kazi kwa nguvu zote, wananchi wana shida kubwa, sisi tuliopewa dhamana tumsaidie Rais," Jafo aliagiza.

## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Yono Auction Mart and Company Ltd & Adili Auction Mart Ltd** Kwa idhini tuliyopewa na **AMANA BANK LTD** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa wadaiwa wote na wadhamini mlipe madeni yenu yote kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. Mnada utafanyika mahali ilipo dhamana.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA NA MAHALI ILIPO**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA INAYOUZWA | MAHALI DHAMANA ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA | MUUZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ROBIN KITAMBALI MPALANG'OMBE | TOYOTA IST, NAMBA ZA USAJILI T 860 DQB | Yono Auction Mart Yard - Bahari Beach Area | Tarehe 03.08.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Yono Auction mart Mawasiliano simu: 0767 675 168 |
| 2 | CHIYENGELE DOTO MKAMA | TOYOTA ALLEX, NAMBA ZA USAJILI T208 DQP | Yono Auction Mart Yard - Bahari Beach Area | Tarehe 03.08.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Yono Auction mart Mawasiliano simu 0767 675 168 |
| 3 | GREYSON LAZARO KAYUMBA | TOYOTA IST, NAMBA ZA USAJILI T 986 DRD | Yono Auction Mart Yard - Bahari Beach Area | Tarehe 03.08.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Yono Auction mart Mawasiliano simu 0767 675 168 |
| 4 | GRANITECH (T) COMPANY LIMITED | T 384 DJH HYDRAULIC CRAWLER | Yono Auction Mart Yard - Bahari Beach Area | Tarehe 03.08.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Yono Auction mart Mawasiliano simu 0767 675 168 |
| 5 | MZEE YUSSUF ENTERPRISES | C.T No. 143856 L.O No. 484338 | Plot No 53, Block 'Q' Buyuni Area, Ilala Municipality | Tarehe 13.08.2020 Saa 8:00 mchana na kuendelea | Yono Auction mart Mawasiliano simu 0767 675 168 |
| 6 | MZEE YUSSUF ENTERPRISES | C.T No. 123674 L.O No. 486639 | Plot No 1002, Block 'AA' Mbagala Area, Temeke Municipality | Tarehe 13.08.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Yono Auction mart Mawasiliano simu 0767 675 168 |
| 7 | GRANITECH (T) COMPANY LIMITED | C.T No. 104135 L.O No. 331861 | Plot No 2185, Block 'D' Mbezi beach Area, Kinondoni Municipality | Tarehe 07.08.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Adili Auction Mart Mawasiliano 0767873988 |
| 8 | GRANITECH (T) COMPANY LIMITED | C.T No. 15397 L.O No. 395191 | Plot No 2186, Block 'D' Mbezi beach Area, Kinondoni Municipality | Tarehe 07.08.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Adili Auction Mart Mawasiliano 0767873988 |
| 9 | GRANITECH (T) COMPANY LIMITED | C.T No. 84598 L.O No. 396695 | Plot No 319, Ex Daya Estate, Ilala Municipality | Tarehe 07.08.2020 Saa 8:00 mchana na kuendelea | Adili Auction Mart Mawasiliano 0767873988 |
| 10 | NYAMWESE GROUP LTD | Residential License No. KND 011354 Parcel No. KND/KWE/MLK23/62 | Mlalakuwa Street, Kawe, Kinondoni Municipal ity | Tarehe 09.08.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Adili Auction Mart Mawasiliano 0767873988 |
| 11 | MWALULAS GENERAL SERV. & SUPPL. CO.(T) LTD | C.T No. 86064 L.O No. 397139 | Plot No 157, Block 'F' Ukonga Area, Ilala Municipality | Tarehe 09.08.2020 Saa 8:00 mchana na kuendelea | Adili Auction Mart Mawasiliano 0767873988 |

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
2) Ukaguzi wa dhamana utafanyika siku nne kabla ya mnada kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana.
3) Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4) Dhamana itauzwa " **kama ilivyo**"

**WOTE MNAKARIBISHWA**

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**MKURUGENZI MTENDAJI,
YONO AUCTION MART AND COMPANY LTD,
JENGO LA MAVUNO, MTAA WA AZIKIWE
S L P 10674,
DAR ES SALAAM**


**MKURUGENZI MTENDAJI,
ADILI AUCTION MART LTD,
JENGO LA ALWAHDA, MNAZI MMOJA
S L P 40616,
DAR ES SALAAM**

**AU Mkurugenzi Mtendaji
Amana Bank Ltd
P.O. BOX 9771
DAR ES SALAAM
TEL: +255 (022) 2129013**

# Sura mpya zamiminika ubunge CCM


Ummy Mwalimu- Tanga Mjini.


Deogratius Nsokolo-Nsimbo



Abdallah Zome- Songea Mjini


Shyrose Bhanji-Viti Maalum mkoa wa Dar es Salaam

**Na Waandishi Wetu**

SURA mpya zimeendelea kujitokeza katika mchakato wa kuwania ubunge kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Katika Jimbo la Kawe, Nipashe jana ilishuhudia aliyekuwa Katibu Makuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Dk. Vincent Mashinji, akichukua fomu kuomba ridhaa ya CCM kuteuliwa kukiwakilisha chama tawala kuchuana na aliyekuwa mbunge wake, Halima Mdee.

Wengine waliojitokeza kulisaka jimbo hilo ni mjukuu wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Magori Nyerere, maarufu kama Sophia, na Ofisa Rasilimali na Mshauri wa Majanga wa Benki ya NMB, Pascal Itangaja.

Katika Jimbo la Kinondoni, aliyekuwa mbunge, Maulid Mtulia, alichukua na kurejesha fomu, sawa na mbunge wa zamani wa jimbo hilo, Idd Azzan aliyechukua jana na kurejesha muda mfupi baadaye.

Wengine waliochukua fomu kuwania ubunge Kinondoni ni Wangota Salum na daktari wa Hospitali ya Magomeni, William Barinzigo.

Katika Jimbo la Temeke, waliorudisha fomu jana, ni aliyekuwa mbunge wake Abdallah Mtolea, huku Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, akirejesha fomu kuwania ubunge wa Ilala.

Sura nyingine mpya kwa jana ni Msemaji wa Yanga, Antonio Nugaz, aliyechukua fomu kuomba kuteuliwa Jimbo la Segerea na Mchekeshaji Sylivester Mjuni 'Mpoki' aliyechukua fomu kuwania Jimbo la Kigamboni.

Wilayani Nzega mkoani Tabora, makada 16 wa CCM wamejitosa kuwania ubunge katika Jimbo la Nzega Vijijini, akiwamo aliyekuwa mbunge wake na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla.

Katika Jimbo la Nzega Mjini, wanachama wanane wa CCM wamejitosa kuomba kuteuliwa kuwania ubunge wa jimbo hilo akiwamo Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, huku makada 24 wakichukua fomu kusaka Jimbo la Bukene.

Wilayani Igunga mkoani Tabora, aliyekuwa Mbunge wa Manonga katika Bunge la 11, Seif Gulamali, jana alichukua na kurejesha fomu kuomba kuteuliwa na CCM kuwania tena ubunge wa jimbo hilo.

Katibu wa CCM wilayani Songea, Juma Mperi, aliiambia Nipashe jana kuwa, makada 26 wamejitokeza kusaka nafasi ya kuwania ubunge wa Songea Mjini, akiwamo aliyekuwa mbunge wake, Dk. Damas Ndumbaro, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dk. Tasco Luambano, Dk. Tereza Uvisa na aliyekuwa Kamishna Msaidizi wa Polisi Abdallah Zombe.

Kwenye Jimbo la Madaba, makada saba, akiwamo aliyekuwa mbunge wake, Joseph Mhagama wamechukua fomu huku Jimbo la Peramiho likiwavuta makada watano, akiwamo aliyekuwa mbunge wake na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jenista Mhagama.

Wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, Jimbo la Mbinga Mjini limewavutia makada 16 akiwamo aliyekuwa mbunge wake, Sixtus Mapunda wakati Mbinga Vijijini wanachama 18 wamejitokeza kuchukua fomu, wakiwamo makatibu tawala wawili wastaafu Dk. John Ndunguru na Adolati Mapunda.

Kada wa zamani wa CHADEMA, James Lembeli, amejitosa kuwania ubunge wa Kahama Mjini kupitia CCM, akitamba 'kupambana na vijana'.

***Imeandikwa na Magdalena Haule, Mary Mshami na Fatma Mtutuma (DAR) na Gideon Mwakanosya (SONGEA)**


Christopher ole Sendeka- Simanjiro


Sylvester Mujuni 'Mpoki'- Kigamboni.


James Lembeli- Kahama Mjini


Dk. Vicent Mashinji-Kawe

# DC aliyetumbuliwa aanika sababu za kuwania ubunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Deogratius Ndejembi, ametaja sababu ya iliyomsukuma kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya kugombea ubunge wa Jimbo la Chilonwa.

Ndejembi aliteuliwa mwaka 2016 kutumikia Wilaya ya Kongwa, lakini juzi Rais John Magufuli alimteua Dk. Seleman Serera kuwa mkuu wa wilaya hiyo.

Baada ya kurejesha fomu jana kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi(CCM) kuteuliwa kuwania ubunge katika jimbo hilo, Ndejembi alisema alichukua uamuzi huo kutokana na kuombwa na wananchi, hasa wazee wa jimbo hilo.

"Wakati nipo kwenye ukuu wa wilaya, wananchi wengi, wazee wengi walisema 'kwanini usirudie kujaribu?' Mwaka 2015 nilishika nafasi ya pili kwenye kura za maoni, tena kwa tofauti ya kura chache sana kipindi hicho.

"Pia, ninataka kuendeleza kasi ya Rais ya kuwanyanyua watu kwenye uchumi wa kati ambao tumeshaufikia. Nimeona niingie kwenye kinyang'anyiro hiki na nipo tayari kwa matokeo yoyote maana asiyekubali kushindwa si mshindani na wakati ninatafakari uamuzi wangu wa kugombea, niliona pande zote mbili yaani kushinda na kushindwa," alisema.

"Dhamira yangu ni ileile ambayo Rais aliiona na kuniteua kuwatumikia wananchi hasa wa hali ya chini, ili kuleta mabadiliko makubwa na kasi ileile ambayo Rais anaitaka. Katika miaka minne ya ukuu wa wilaya, dhamana niliyopewa na Rais imenifunza vitu vingi katika kuhudumia wananchi.

"Nilipata fursa na bahati kuwa kwenye wilaya inayofanana kabisa na changamoto za jimbo ninaloomba kuteuliwa kugombea la Chilonwa. Katika Watanzania zaidi ya milioni 55 kuchaguliwa mimi kuwa DC ni jambo kubwa sana.

"Sitakuja kulisahau katika maisha yangu na historia yangu kwamba nilipata fursa kutumikia nchi yangu, katika kipindi ambacho yalikuwa yakifanyika mabadiliko makubwa ambayo yamebadili vitu vingi na kuwa vitu chanja ndani ya taifa letu," alisema.

**MAKADA 51 JIMBO MOJA**

Wakati mchakato wa uchukuaji na urejeshaji fomu ukiendelea ndani ya CCM, hadi jana jioni, kulikuwa na makada 51 waliokuwa wamechukua fomu kuomba kuteuliwa Jimbo la Dodoma Mjini.

Kati yao, yumo aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, ambaye alisema kuwa miaka mitano iliyopita na mafanikio yaliyopatikana, yamempa ari zaidi ya kuwatumikia wananchi.

Katika Jimbo la Bahi, wanachama 36 walikuwa wamechukua fomu hadi jana jioni, huku makada 18 wakijitosa Jimbo la Mtera na wengine 10 wakichukua fomu Jimbo la Kongwa 10, akiwamo Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Katika Jimbo la Chilonwa, makada 30 walikuwa wamechukua fomu hadi jana jioni, 16 wakirejesha, huku 18 wakijitosa katika Jimbo la Kibakwe. Jimbo la Mpwapwa limevutia makada 57, huku 35 wakirejesha fomu. Kwenye Jimbo la Kondoa, wanachama 12 wa CCM walikuwa wamechukua fomu hadi jana jioni, huku Kondoa Mjini wakijitokeza makada 45 na wengine 34 wakichukua fomu kusaka Jimbo la Chemba.



Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Christine Musisi (kulia), akikabidhi msaada wa vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya Sh. milioni 160 kwa Mwenyekiti wa Tume za Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu kwa ajili ya matumizi ya ofisi hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# UNDP yaifagilia Tanzania kuingia uchumi wa kati

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SHIRIKA la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) limeipongeza Tanzania kwa kufanikisha nchi kufika uchumi wa kati kabla ya 2025 kama ilivyokuwa ikitarajiwa.

Hivi karibuni Benki ya Dunia ilitangaza kuwa Tanzania imekuwa ni miongoni mwa nchi zilizomo katika uchumi wa kati kwa kundi la chini.

Akizungumza jana jijini hapa wakati akikabidhi vifaa vya TEHAMA kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nchini, Mwakilishi Mkazi wa UNDP nchini, Christine Musisi, aliipongeza serikali kwa kufikia mafanikio hayo.

"Sisi UNDP tunaipongeza Serikali ya Rais John Magufuli kwa jitahada ilizofanya na kuipeleka Tanzania kuwa moja ya nchi zilizomo katika uchumi wa kati kabla ya 2025 kama ilivyokuwa ikitarajiwa," alisema Musisi. Aidha, mwakilishi huyo mkazi alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika masuala ya maendeleo kwa kufanya miradi mikubwa kwa kutumia vyanzo vya fedha za ndani.

Katika hatua nyingine, Musisi alimpongeza Rais Magufuli kwa kupambana na ugonjwa wa corona, hivyo kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi hivyo. "Kwa kweli tunaipongeza serikali chini ya Dk. Magufuli kwa kufanya jitihada kubwa za kupunguza ugonjwa wa corona, jambo ambalo limeonekana kufanikiwa kwa kiasi kikubwa," alisema mwakilishi huyo.

Musisi alisema UNDP kwa kutambua mchango mkubwa wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nchini, imetoa msaada wa vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya Sh. milioni 160 kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa kazi wa tume hiyo.

"UNDP tunatambua mchango wa Tume ya Haki za Binadamu nchini, ndio maana tumetoa msaada huo ili kuunga juhudi za kazi ya tume hiyo nchini," alisema Musisi.

# Viongozi dini wataka wanawake kuwania

**Na Halfani Chusi**

VIONGOZI wa dini wametoa wito kwa wanawake kujitosa kuwania nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu baada ya kubaini kundi hilo limeachwa nyuma kwenye mchakato wa uchaguzi huo.

Rai hiyo ilitolewa jana wakati wa uzinduzi wa mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa kamati za uhusiano na ushirikiano wa viongozi wa dini nchini, uliohudhuriwa na viongozi kutoka Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA), Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC) na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) jijini Dar es Salaam.

Padri Charles Kitima, akizungumza kwa niaba ya viongozi wenzake wa dini, alisema viongozi wa dini wanapaswa kuhamasisha wanawake wajitose katika uchaguzi huo kwa kuwania nafasi mbalimbali.

"Kutokana na mila na desturi zetu, wanawake wamekuwa wakibaguliwa sana katika nyanja mbalimbali za uongozi, kudharauliwa na hata kutokupewa kipaumbele katika nyadhifa wakati hata Biblia inakataa hilo.

"Ndiyo maana tumeona sisi viongozi wa dini tuungane kwa pamoja, ili kupeana elimu tukasaidiane kuelimisha wenzetu mitaani huko, ili kuchochea maadili na amani kama ambavyo yanasema mafundisho ya dini," alisema.

Askofu Nelsoni Kisale alisema kuwa mbali na kuhamasisha wanawake kujitosa katika uchaguzi huo, pia wana jukumu la kuitaka jamii ichagua viongozi wenye hofu ya Mungu. "Viongozi wenye hofu ya Mungu ndiyo watakaoleta maendeleo nchini na si vinginevyo. Hao ndiyo watasababisha uwapo wa amani pamoja na utendekaji wa haki katika sekta mbalimbali za uongozi nchini.

"Mara nyingi tunapochagua kiongozi asiye na hofu ya Mungu lazima huwa tunaingia katika migogoro isiyo ya lazima, hii yote ni kutokana na kukosa viongozi wenye hofu ya Mungu.

"Tukichagua viongozi wenye hofu na Mungu, itatusaidia kuinua zaidi hata uchumi wa nchi kwa kuwa watafanya kazi kwa kujali maslahi ya umma na siyo maslahi binafsi," alisema.

Sheikh Mohamed Khamisi kutoka BAKWATA, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa baraza hilo, alisema mafundisho ya dini yanahimiza mwanamke kupewa kipaumbele katika nafasi za uongozi.

"Muda mwingi mwanamke

# Zungu kusaidia kiwanda kupata malighafi

**Na Mwandishi Wetu,**
MUKURANGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira),Mussa Zungu, ameahidi kutatua changamoto ya upatikanaji wa chuma chakavu ili kuhakikisha uzalishaji katika kiwanda cha Lodhia Steel Industries Limited hausimami kwa sababu ya kukosa malighafi ambayo inapatikana kwa wingi nchini.

Akizungumza na wanahabari jana, baada ya kukagua na kusikiliza maelezo ya Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Sailesh Pandit, Waziri Zungu alisema serikali inatambua umuhimu wa kiwanda hicho na kuahidi kuwasiliana na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), ili kupata utaratibu mzuri wa wajasiriamali kuviuzia viwanda vyuma chakavu bila usumbufu.

"Napenda kuwaahidi kwamba serikali inatambua mchango wenu. Na kuhusu changamoto hii tutakaa na maofisa wa NEMC na kuweka utaratibu mzuri ambao utarahisisha upatikanaji wa vibali kwa haraka zaidi," alieleza Waziri Zungu.

Waziri amekipongeza kiwanda kwa kutengeneza bidhaa zenye ubora ambazo zinauzwa nchini na pia kuuzwa katika nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Burundi.

"Niseme wazi kabisa, nyinyi hapa mnatekeleza vyema azma ya Rais John Magufuli ya kujenga Tanzania ya Viwanda kwa vile mitambo niliyoiona inakidhi sifa za kiwanda hiki kuitwa kiwanda kikubwa nchini," alisema Waziri Zungu.

Amekipongeza kiwanda hicho kwa kuyatunza mazingira na kuwasihi waendelee kutunza mazingira hayo.

"Kwa kweli nimefuraishwa sana na mazingira niliyoyaona kwenye kiwanda hiki, na napenda kuwahimiza mwendelee kuyatunza mazingira haya," alisema Zungu.

Pandit aliiomba serikali kutatua haraka changamoto ya upatikanaji wa vibali kwa wachuuzi wa vyuma chakavu ili kiwanda kiweze kuendelea na uzalishaji kama inavyotarajiwa.

SUKAH SECURITY CO. (T) LTD
AUCTION MART & COURT BROKER
(WATU WA KAZI)

HEAD OFFICE:
P.O. Box 10751, DVN Building,
Posta Road Mwanza.
Mob: 0754 860 435, 0715 860 435

Dealers in:
Day and Night Safe Guards,
Security Consultants,
Rapid Ambulance response,
Dog Unit and Mobile Patrolling,
Debt collector and General Auctioneers

KAGERA BRANCH:
P.O. Box 574,
Mobile: 0754 860 435
KARAGWE.

NOTICE /TANGAZO

KWA IDHINI YA TULIYOPEWA NA **KCB BENK SUKAH SECURITY COMPANY LIMITED** TUTAUZA KWA NJIA YA ADHARA NYUMBA ZA WADAIWA WA BENK KAMA IFUATAVYO:-

| NA | DHAMANA | TAREHE/ SIKU | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | PLOT NO. 421 BLOCK 'HH' NYAKATO | 08/08/2020 JUMAMOSI | 4:00 ASUBUHI |
| 2. | PLOT NO. 431 BLOCK 'A' NYASAKA | 08/08/2020 JUMAMOSI | 6:00 MCHANA |
| 3. | PLOT NO. 198 BLOCK 'E' NYASAKA | 08/08/2020 JUMAMOSI | 8:00 MCHANA |
| 4. | PLOT NO. 384 BLOCK 'LL' KILOLELI | 09/08/2020 JUMAPILI | 4:00 ASUBUHI |
| 5. | PLOT NO. 71 BLOCK 'AVI' KIRUMBA MWANZA-CITY | 09/08/2020 JUMAPILI | 6:00 MCHANA |
| 6. | PLOT NO. 340 BLOCK 'J' NYAMANORO – MWANZA – CITY | 09/08/2020 JUMAPILI | 8: 00 MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA**
MNUNUZI ANATAKIWA KULIPA ASIMILIA 25% PAPO HAPO NA ASIMILIA 75% ILIPWE NDANI YA SIKU (14). NYOTE MNAKARIBISHWA

KWA MAWASILIANO ZAIDI 0754 – 860 435

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunataka usalama wa uhakika kwa wote kuelekea uchaguzi

**WAKATI** michakato ikiendelea katika vyama vya siasa kwa ajili ya uteuzi wa makada wao watakaopeperusha bendera za vyama hivyo, tunaona kuwa serikali inawajibika kuanza kuimarisha usalama.

Kuna umuhimu wa kuwapo kwa usalama wa kutosha kwa kuwa uzoefu tulionao unaonyesha kuwa wakati wa uchaguzi ndipo hutokea matukio zaidi ya uhalifu, ambayo hutishia wananchi na mali zao. Kuna uhalifu ambao hufanywa na majambazi kwa kutumia kivuli cha uchaguzi kwa lengo la kutekeleza malengo yao husuan ya kupata fedha na mali.

Pia wakati wa kuelekea kwenye uchaguzi hutokea makundi ya yenye mrengo wa kisiasa ambayo hufanya matukio ya vurugu, ikiwamo kuvunja mikutano ya vyama, kushambulia na kujeruhi viongozi, wananchama na wafuasi wa vyama.

Vilevile, kuna makundi katika jamii hususan ya waganga wa kienyeji, ambao huibuka kipindi kama hiki na kuwashauri baadhi ya wanasiasa namna ya kushinda katika uchaguzi.

Waganga hao wamekuwa wakilalamikiwa kwa muda mrefu kwa kuhatarisha amani kwa kuwadanganya watu wenye nia ya kugombea uongozi kutekeleza masharti ambayo ni ya kihalifu.

Kwa mfano, yamekuwapo madai kuwa wenye nia ya kugombea wamekuwa wakidanganywa kujihusisha na vitendo vya ushirikina kama kuuziwa viungo vya binadamu hususan watu wenye ualbino pamoja na mambo mengine ya ovyo kama hayo.

Kutokana na elimu ndogo na kushindwa kujitambua, baadhi ya wagombea uongozi wa kuchaguliwa kama ubunge na udiwani wamekuwa wakikubali kutekeleza masharti hayo, hivyo kuwa kichocheo cha mauaji katika jamii.

Huko nyuma tulishuhudia kasi ya watu hususani wenye ulemavu wakiuawa katika baadhi ya mikoa kutokana na imani potofu za kupata uongozi pamoja na utajiri.

Kutokana na hali hii, ndiyo maana tunaona kuwa sasa ni wakati mwafaka kwa serikali kuvielekeza vyombo vyake vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi kuanzia sasa ili kuweka mazingira bora kuelekeza katika uchaguzi mkuu ambao unatarajiwa kufanyika Oktoba. Hatua hiyo itawawezesha Watanzania wote kutimiza haki yao ya kushiriki kuchagua na kuchaguliwa bila kuwa na hofu yoyote kuhusiana na usalama wao.

Baada ya mchakato wa uteuzi ndani ya vyama kisha wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), hatua itakayofuata ni ya kampeni kwa ajili ya vyama na wagombea kunadi sera, mikakati na mipango yao kwa wananchi kwa lengo loa kuchaguliwa.

Kipindi cha kampeni ni wakati muhimu sana katika uchaguzi kwa kuwa vyama na wagombea wanakuwa na shughuli nyingi zikiwamo za kuzunguka maeneo mengi kufanya mikutano, hivyo kuhitaji ulinzi wa kutosha wa vyombo vya dola.

Ikumbukwe pia kuwa nchi yetu ni kubwa kwa eneo, hivyo kuna haja ya kila maeneo kuwapo na askari hususan Polisi wa kutosha, ili wagombea wa ngazi zote pamoja na wafuasi wao wafanya kampeni zao kwenye mazingira yenye amani na usalama.

Tunaamini kuwa Jeshi la Polisi litakuwa limeshajipanga kwa ajili ya kuhakikisha kuwa ulinzi ni wa uhakika nchi nzima, na kwamba hakuna kundi ambalo litatishiwa wala kudhurika wakati wote kuelekeza uchaguzi Oktoba. Tunaona kuwa itakuwa vizuri kama viongozi wa Jeshi la Polisi watafanya vikao na waganga wa tiba asilia na mbadala katika maeneo yao ili kuwakumbusha wajibu wao na kuwatahadharisha wasijihusishe na vitendo vya ramli chonganishi pamoja na kuweapa wanasiasa masharti ambayo yanaweza kusababisha uvunjifu wa amani, yakiwamo mauaji ya watu wenye ulemavu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wenye malori Mkuranga ajirini madereva wenye uweledi kazini

Na Yasmine Protace, MKURANGA

**AJALI** za barabarani zinapotokea na kusababisha vifo au kuleta ulemavu wa aina yoyote kwa mwanadamu, kunafanyika tathmini kubwa kutoka chanzo hadi kufikwa ajali hiyo.

Tumekuwa tukisikia ajali nyingi zinapotokea, utaambiwa mwendo wa gari ulikuwa sio mzuri au utasikia dereva alikuwa akikimbiza gari na bahati mbaya akasababisha ajali.

Sababu nyingi zimekuwa zikitajwa kuchangia, lakini zipo zinazotokana na miundombinu duni katika kipindi cha mvua, hata kusababisha magari kuachia njia na kutumbukia katika mito.

Hadi sasa kumekuwapo taarifa zinazotolewa zenye madai kwamba, hata madereva nao kuna walikosa sifa na kuendesha magari hayo wakiishia kusababisha ajali.

Sote ni mashahidi wa Polisi wa Usalama Barabarani, kwa kushirikiana na wadau wengine, mbali na kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu huko waliko, pia hawachoki kupaza sauti za elimu na tahadhari kuanzia kwa dereva na watumiaji huduma hizo.

Ni hadithi ambayo bado haijafifia, leo hii miaka imetimu miwili wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, kuwapo mkasa wa gari la kubeba mchanga liligonga gari dogo la abiria aina ya Toyota Hiace na kusababisha ajali ya watu 14 wa familia na kati yao wapo waliokutwa na umauti.

> **Ni hadithi ambayo bado haijafifia, leo hii miaka imetimu miwili wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, kuwapo mkasa wa gari la kubeba mchanga liligonga gari dogo la abiria aina ya Toyota Hiace na kusababisha ajali ya watu 14 wa familia na kati yao wapo waliokutwa na umauti.**

Kutokana na tukio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Injiani Evarist Ndikilo, alizuia malori ya kubeba mchanga kusafirisha mzigo huo usiku.

Ni maagizo yaliyowataka wachimba mchanga na wasafirishaji wake, kuifanya kazi hiyo mwisho saa 12 jioni, muda wa kuanza saa12 asubuhi. Yaani wanatumika kwa saa 12.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, anasema utaratibu wa kuruhusu wenye magari ya mchanga kufanya kazi kwa saa 24 unaendelea kuandaliwa.

Sanga anasema, uongozi wa Mkoa wa Pwani unaendelea kuweka sawa utaratibu, ili kuwaruhusu tena wasafirishaji kufanya kazi yao kwa mzunguko wa siku nzima. Anasema, pamoja na utaratibu kuandaliwa, anawataka wenye malori kuajiri waendeshaji walio na sifa na kuwapo madereva wawili watakaosaidiana muda wote.

Kiongozi huyo mkuu wa serikali katika wilaya hiyo, anasema polisi limejipanga kuhakikisha inatoa elimu sahihi kwa madereva wanaosafiri na magari hayo wawe na sifa kamili.

"Mlishuhudia ajali iliyotokea mwaka juzi na kuua watu 14 wa familia moja. Sababu ya ajali ilielezwa ni lori la mchanga kuigonga (Toyota) Hiace iliyokuwa imebeba familia hiyo," anasema. Anaongeza kuwa tukio hilo la ajali lilitokea usiku, hivyo Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Injinia Ndikilo alilazimika kuzuia usafirishaji mchanga muda wa usiku.

Sanga anasema, ni muhimu wamiliki wa malori hayo wakahakikisha wanaajiri madereva walio na sifa zinazokubalika.

Mkuranga ni wilaya inayopitiwa na barabara kuu kati ya Dar es Salaam na mikoa ya Kusini, Lindi na Mtwara na kabla ya kujiunga na mkoa Lindi, Mkuranga inatenganishwa na Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, wakati Dar es Salaam, inapakana nayo katika Wilaya ya Temeke.

# Kampuni yasaidia 1,000 upasuaji mabusha, ngiri

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Equinor ya Tanzania imefanikiwa kuwasaidia wagonjwa 1,000 wenye mabusha, matende na ngiri maji kufanyiwa upasuaji mkoani Lindi.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa kambi ya matibabu hayo, Naomi Makota, kutoka Equinor alisema kampuni hiyo imekuwa ikifadhili wagonjwa wa aina hiyo kwa miaka sita mfululizo.

Alisema kampuni hiyo imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kitengo chake kinachokabiliana na magonjwa yasiyopewa kipaumbele. Kambi inayoendelea hivi sasa ilianza Jumatatu wiki hii na inatarajiwa kumalizika siku ya Jumanne tarehe 21 mwezi huu, ambapo jumla ya wagonjwa 170 watapatiwa huduma hiyo.

Naomi alisema mradi huo ambao ulianzia katika Mkoa wa Mtwara mwaka 2015 na baadaye kutekelezwa mkoani Lindi kuanzia mwaka 2017.

Alisema mradi huo umekuwa ukipatiwa msaada wa Equinor kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH). Aidha, Naomi alisema madaktari hao wamekuwa wakiweka kambi katika Hospitali ya Rufani ya Sokoine mkoani Lindi na kufanya upasuaji wa wagonjwa wa mabusha na ngiri (hernia).

"Equinor na wadau wote katika mradi huu wanafurahia mafanikio ambapo kwa mfululizo wa miaka sita, wameweza kuwafikia wagonjwa zaidi 1,000 na kufanyiwa upasuaji huo na kwa wiki hii wagonjwa 170 wanatarajiwa kupata huduma hii," alisema. Alisema kampuni ya Equinor inajisikia faraja kwani kupata matibabu kwa wagonjwa hao kunaondoa mzigo kwa familia zao nao pia wanaweza kushiriki kufanya kazi na kuleta maendeleo katika jamii. Naoni alisema kwa kipindi cha miaka sita ya utekelezaji wa mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 500 za Tanzania ambazo ni msaada kutoka Equinor.

Equinor ni kampuni ya nishati yenye makao makuu katika mji wa Stavanger, nchini Norway na kwa hapa nchini inaendesha kitalu namba mbili cha gesi ikishirikiana na ExxonMobil na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).



Aliyekuwa Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali, akichukua fomu ya kuomba ridhaa ya CCM kuwania tena ubunge wa jimbo hilo, kutoka kwa katibu wa chama hicho Wilaya ya Igunga, Mwanamvua Killo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sekta binafsi yapata bosi mpya

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imemteua Zacky Mbenna kuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, rasmi kuanzia Julai 15, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na taasisi hiyo jana na kusainiwa na Mwenyekiti wake, Angelina Ngalula, kabla ya uteuzi huo, Mbenna ambaye ni mzoefu katika masuala ya usimamizi wa biashara na utawala alikuwa Mkurugenzi wa Huduma ya Wanachama wa taasisi hiyo.

Taarifa hiyo ilisema kuwa uteuzi huo umefanywa kufuatia kujiuzulu kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji, Godfrey Simbeye, ambaye amehudumu kwenye taasisi hiyo kwa zaidi ya miaka 10.

"Kwa mara nyingine tena, Bodi ya Wakurugenzi inapenda kumshukuru Simbeye kwa kujitoa kwake katika kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa sekta binafsi nchini," alisema Ngalula katika taarifa hiyo.

Ngalula aliwahakikishia wanachama wote, serikali, wabia wa maendeleo kuwa katika kipindi hiki cha mpito, mamlaka na shughuli za taasisi zitaendelea kama kawaidi pasipo kuathirika.

TPSF ni mbia mkubwa wa serikali na wadau wengine katika kuandaa na kutekeleza sera na mikakati inayolenga kuchochea ukuajia na maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika Tanzania.

Taasisi hiyo pia ni sauti ya sekta binafsi na mwamvuli wa vyama na mashirika katika sekta binafsi kwenye sekta za kiuchumi nchini.

# Wanachama 20 wampinga Adadi

**Na Steven William,** MUHEZA

MAKADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliochukua fomu ya kuomba kuteuliwa na chama hicho kugombea ubunge Muheza mkoani Tanga, wamefikia 20, huku msanii wa muziki wa kizazi kipya, Hamisi Mwinjuma, maarufu Mwana FA, akiwa miongoni mwao.

Katibu wa CCM Wilaya ya Muheza, Mohamed Moyo, aliiambia Nipashe jana kuwa, mbali na Mwana FA, makada wengine wa chama hicho waliokuwa wamejitokeza ni pamoja na aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo katika Bunge la 11, Balozi mstaafu Adadi Rajabu.

Aliwataja makada wengine kuwa ni pamoja na Dk. David Mwendamaka, Hassan Msumari, Asha Wandi, George Semnga, Peter Zaghara, Juma Juma na Ramadhani Bakari. Moyo alisema vijana wengi na wanawake wamejitokeza kugombea nafasi ya ubunge na udiwani katika Wilaya ya Muheza, akipongeza mwamko huo.

"Bado makada zaidi wa chama wanaendelea kuja kuchukua fomu za ubunge, lakini idadi ya vijana inatia moyo," alisema.

Moyo alisema kuwa katika kata mbalimbali vijana wengi wamejitokeza kutangaza nia ya kugombea udiwani wakiwamo vijana waendesha pikipiki, maarufu bodaboda na mama lishe.

# Mtoto afa kwa kuangukiwa mbuyu

**Na Said Hamdani,** LINDI

MTOTO Faridi Simba (5), wa Kitongoji cha Ruo, Kijiji cha Kiwalala, Mkoa wa Lindi, amefariki baada ya kuangukiwa na mti aina ya mbuyu.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Stanley Kulyamo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuelezea kwamba tukio hilo lilitokea juzi nyakati za usiku.

Alisema wakati mbuyu huo unaanguka, mama wa mtoto huyo alikuwa anaingia ndani kuchukua unga kwa ajili ya kupika chakula cha usiku.

Alisema kitendo cha mama huyo kuingia ndani, mbuyu ulianguka na kufikia paa la nyumba yao na kuwakandamiza watoto, kupoteza uhai wa mtoto huyo na kumjeruhi mtoto mwingine.

Mashuhuda wa ajali hiyo walimtaja mtoto aliyepona kuwa ni Sabria Simba (8) anayesoma Shule ya Msingi Ruo na kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya Sokoine mjini hapa.

Mashuhuda Isumaili Dadi, Yusufu Kimondo na Issa Selemani, walilieza Nipashe kuwa watoto hao walikandamizwa na mbuyu huo, walipokuwa uwanja wa nyumba yao wakicheza.

Walisema mwili wa marehemu uliondolewa baada ya kukata mbuyu kwa kutumia msumeno wa moto aina ya chensoo. "Huyu mtoto Farida alifariki hapo hapo na tulilazimika kutumia msumeno wa chensoo ndipo tukafanikiwa kuuondoa," alisema Selemani.

Baba wa watoto hao, Juma Simba, alisema siku hiyo ya tukio, watoto wake walikuwa wakicheza uwanjani huku wakisubiri mama yao awapikie chakula, ndipo mti huo ulipoanguka na kuwakandamiza na kusababisha kifo cha mtoto Farida.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yaokoa mil. 35/- za wakulima

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imeokoa Sh. milioni 35 kati ya Sh. milioni 394.15 ambazo ni fedha za malipo ya korosho kwa wakulima mkoani Pwani.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya kiutendaji ya miezi mitatu ya taasisi hiyo.

Alisema, wameokoa kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Kampuni ya Mafubilo General Supplies ya jijini Dar es Salaam iliyonunua korosho za wakulima kwa mkopo kupitia Vyama vya Msingi vya Amcos Visiga, Kongowe, Mwendapole, Mkombozi na Miembe saba zenye thamani ya Sh. milioni 394.15.

Raymond alisema malipo ya korosho hizo yalisuasua hadi pale TAKUKURU ilipoingilia kati na kufuatilia kuhakikisha mnunuzi anawalipa wakulima.

Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema, mdaiwa amepewa maagizo ya kulipa hadi kumaliza deni lote analodaiwa ili wakulima wapate haki yao.

Katika hatua nyingine, taasisi hiyo imeokoa Sh. milioni 4.9 za Mwalimu mstaafu, Yusuph Kimweri, ambaye alikuwa amemlipa Ibrahim Masawe, kupitia mkopo usiofuata kanuni, taratibu na sheria zinazosimamiwa na taasisi za fedha nchini kiasi cha Sh. 700,000 alizokopa mwaka 2018.

Akiongelea suala hilo, Suzana alisema kupitia riba deni lilikua na kufikia Sh. milioni 13 ambalo mstaafu huyo alilipa baada ya kupokea pensheni ya kustaafu Mei 27, 2020.

Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema, baada ya kupokea malalamiko hayo walifanya uchunguzi wa kina na kubaini mtuhumiwa alifanya biashara ya kukopesha fedha kinyume na kanuni.

Imeelezwa kuwa baada ya mtuhumiwa kutambua kosa aliahidi kurejesha fedha hizo, kwamba hadi sasa amerejesha Sh. milioni 4.9 na atatakiwa kukamilisha kiasi kilichobaki cha Sh. milioni



Baadhi ya wanaume wakiwa wanasubiri kuingia kwa zamu kwenye Hospitali ya Rufani ya Sokoine mkoani Lindi juzi, kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji wa magonjwa ya mabusha na ngiri maji kwa ufadhili wa kampuni ya Equinor. P**ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushirika kuzalisha miche kahawa 23,375

**Na Gedion Mwakanosya, MBINGA**

KAIMU Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Mbinga (MBIFACU), Henrick Ndimbo, amesema katika msimu huu imepanda miche ya kisasa ya kahawa 23,275.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa ifikapo mwaka 2023 wanatarajia kuzalisha kahawa tani zaidi ya 23,000 ambazo zitawaingizia Sh. milioni 69 na kuongeza mapato ndani ya chama.

Akizungumzia historia ya shamba hilo, Ndimbo alisema katika kijiji cha Ugano, wanamiliki eneo la hekari 1,052 na kwamba bado wana shamba la zamani la kahawa lenye ukubwa wa hekari 50.

Alisema walipokabidhiwa miche hiyo kutoka Chama Kikuu cha Ushirika cha MBICU, waliamua kuifufua upya miche hiyo na kuacha baadhi ya miche ya zamani inayotumika kama shamba darasa.

"Hii miche ya zamani ya kahawa ukiitunza vizuri inaweza kutoa hadi kilo tano kwa mche mmoja, msimu uliopita tuliweza kupata hadi tani 2.6 za kahawa kwa miche ya zamani ambazo zilituingizia milioni tisa," alisema Ndimbo.

Naye Kaimu Makamu Mwenyekiti wa MBIFACU, Winfred Lupembe, alisema shamba hilo litaimairisha uchumi wa chama hicho.

Alisema katika shamba jipya, miche ya kahawa imefunikwa kwa majani ili kuilinda wakati wa baridi na wakati wa jua kali isipate mwanga mkali na kuathirika.

"Shughuli zote ambazo tunazifanya MBIFACU zinalenga kuongeza ajira kwa vijana katika Wilaya ya Mbinga, lakini jambo kubwa zaidi ni kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli kwa kauli yake ya kuimarisha ushirika nchini," alisema Lupembe.

Lupembe alisema katika kuliboresha shamba la zamani la kahawa chama hicho kina mpango wa kufuga ng'ombe ambao watawawezesha kupata mbolea ya samadi ambayo itatumika kuweka kwenye kahawa.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Ruvuma, Bumi Masuba, alitoa rai kwa vyama vya ushirika nchini kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ili viwe na vyanzo vingine vya mapato badala ya kutegemea ushuru wa mazao ya mkulima.

## Serikali yawatumia salamu waliokula fedha za wasanii

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya serikali kuhamisha Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, kwenda Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imetuma salamu kwa wale waliokula fedha za wasanii.

Akizungumza na wasanii jana jijini Dar es Salaam juzi, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbasi, alisema wameshaokoa Sh. milioni 200 za wasanii ambazo zilikuwa zimeliwa na wajanja, wakiwamo ambao wamefariki dunia.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 65 zimerejeshwa kwa familia ya aliyekuwa msanii wa vichekesho, marehemu Amri Athuman maarufu kama King Majuto.

Pia alisema Sh. milioni 20 zimerejeshwa kwa familia ya marehemu Steven Kanumba.

Alisema kwa kipindi kirefu fedha za wasanii zilikuwa zinaliwa na wajanja, kwamba kwa sasa nafasi hiyo haitakuwapo.

"Rais John Magufuli amefanikiwa kuhamisha COSOTA ndani ya saa 24 kutoka Wizara ya Viwanda hadi Wizara ya Habari, baada ya kushindikana kwa miaka mingi," alisema Dk. Abbasi.

"Na mimi ndani ya saa 24 zijazo nimepanga kufanya mazungumzo na Bodi ya COSOTA, maana wana matatizo mengi kuliko mikakati, nataka kujua kama hela ya wasanii ambazo zimeliwa ziko wapi maana naskia wengine hawajalipwa miaka miwili, mitatu."

Dk. Abbas pia alisema wamepanga kurejesha viwanja vyote vya sanaa ambavyo vilikuwa vimeporwa katika maeneo mbalimbali.

"Kuna watu wanatubipu, sisi wengine ukitubipu huwa tunapokea. Nafahamu viwanja vingi vya wasanii vimeporwa. Tumeanza kazi ya kuvifukua vyote. Hakuna mahali ambapo mgeni akija kutoka nje anaweza kuwakuta wasanii wamekaa kwa pamoja kwa sababu hawana viwanja," alisema Dk. Abbasi.

"Nataka niwaambie kwamba kwa mtu yeyote aliyechezea vitu vya sanaa, siyo tu kwamba siku zake zinahesabika, siku zake zimekwisha, mtasikia zahama watakalolipata."

Pia alisema wamepanga kumtengeneza msanii ambaye si tu ataishia kuwa maarufu, lakini atakuwa na kipato kupitia kazi zake.

# Wizara yatoa mafunzo kwa wachuna ngozi 700

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KATIKA jitihada za kuhakikisha kuwa thamani ya ngozi inaongezeka, Wizara ya Mifugo na Uvuvi mpaka sasa imetoa mafunzo kwa wachunaji wa ngozi za wanyama takriban 735 nchini.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo, Usalama wa Chakula na Lishe, Gabriel Bura, katika kikao cha wadau wa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (LDF) cha kutathmini athari za ugonjwa wa corona katika tasnia ya ngozi kilichofanyika jijini Dodoma Julai 14, 2020.

Akitoa ufafanuzi kuhusu hatua zinazoendelea kuchukuliwa na wizara katika kuongeza thamani ya zao hilo la ngozi, Bura alisema kuwa mafunzo hayo yametolewa katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Arusha, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Morogoro na Kagera, huku akiongeza kuwa mchakato wa kutoa leseni kwenye mikoa hiyo umeshaanza.

"Pia tumeanza kugawa visu vinavyotakiwa kitaalamu kwa ajili ya kazi ya uchunaji katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara na mchakato wa kuhakikisha vinafika katika kanda zote tulizotoa mafunzo unaendelea," alisema Bura.

Aliongeza kuwa hatua inayosubiriwa ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi kusaini nyaraka za uteuzi wa wakaguzi wa ngozi waliopatikana kutoka kwenye Halmashauri 113 ambao tayari wameshapitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baada ya taratibu kukamilika, wataalamu hao watakuwa na jukumu la kuhakikisha wanasimamia ubora wa ngozi kama walivyoainishwa kwenye Sheria Namba 18 ya Masuala ya Ngozi.

Awali, akizungumza wakati wa kufungua kikao hicho, Mkurugenzi wa Masoko na Uzalishaji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Felix Nandonde, alibainisha kuwa kufuatia ugonjwa wa corona, hivi sasa ngozi inayozalishwa nchini haiendi nje ya nchi na hata kama inaenda sio kwa kiwango kile cha mwanzo.

"Katika kikao hiki mbali na kujadili matumizi ya fedha, pia kitumike kujadili mbinu za kuikwamua tasnia hii ya ngozi kutoka kwenye hali iliyopo kwa sababu mpaka sasa nchi yetu inaagiza zaidi ya jozi milioni 52 za viatu huku uwezo wetu wa kuzalisha viatu ukiwa ni milioni 1.2 tu kwa mwaka," alisisitiza Dk. Nandonde.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) Tawi la Mwanza, Dk. Albert Mmari, alisema taasisi yake ilishaanza kuchukua hatua kadhaa za kuongeza thamani kwenye tasnia ya ngozi ikiwamo kuongeza mashine za mafunzo ya kutengenezea viatu ambapo mpaka sasa zipo 50 ukilinganisha na 25 zilizokuwapo awali.

# Corona yatia hofu walimu kufikia malengo

**Na Happy Severine,** BARIADI

BAADHI ya shule wilayani Bariadi mkoani Simiyu zimeonyesha wasiwasi wa kutofikia malengo zilizojiwekea kutokana na likizo ndefu ya wanafunzi kukaa nyumbani iliyotokana na ugonjwa wa Covid-19.

Hofu hiyo imetokana na wanafunzi wengi wa kuanzia darasa la awali hadi la tatu kusahau vitu vingi walivyokuwa wamefundishwa awali na kuwalazimu walimu kurudia upya kufundisha mada zilizoshafundishwa. Hayo yalisemwa jana na Pendo Manuel, Mwalimu wa Shule ya Msingi Mahaha na kufafanua kuwa tangu walipofungua shule wamekuwa wakipata wakati mgumu wa kurudia mada zilizoshafundishwa kutokana na wanafunzi wengi kusahau masomo waliyokuwa wamefundishwa.

"Changamoto kubwa tunayokutana nayo kwa sasa ni wanafunzi wengi wa darasa la awali mpaka la tatu wamesahau mambo mengi waliyokuwa wamejifunza kabla ya kwenda likizo ya corona, hivyo tunalazimika kuanza upya kufundisha na tunapata hofu kubwa kukamilisha mipango yetu ya kuwa na ufaulu mkubwa," alisema Manuel.

Alieleza kuwa hali hiyo imewafanya walimu wengi kuweka nguvu zao zaidi katika madarasa hayo na kusahau madarasa mengine ambayo nayo yalihitaji msaada wa karibu wa kusoma wakiwa nyumbani. John Makene, mwalimu mkuu msaidizi wa Shule ya Msingi Kidinda, alisema wazazi na walimu walijiwekea malengo ya kupandisha ufaulu wa shule zao, hali ambayo imekuwa tofauti baada ya uwapo wa mlipuko wa Covid-19. "Sio siri sisi walimu tuna hofu kubwa sana kama malengo yetu tuliyokuwa tumejiwekea kama yataweza kufanikiwa kwani likizo ya corona imewafanya wanafunzi wengi kushuka viwango vyao vya uelewa.

Rajab Madaraka, Mwalimu wa Shule ya Msingi Gamondo, alisema unahitajika muda na nguvu za ziada ili shule zifikie malengo zilizojiwekea awali katika kupandisha ufaulu wa shule zao.



Askari wa kikosi cha usalama barabarani akisimamia kuondolewa kwa lori la mizigo lililogongana na lori la kubebea majitaka katika eneo la Tabata Relini, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Uturuki yaionya Afrika kuhusu ugaidi

**Na Enock Charles**

UBALOZI wa Uturuki umezitaka nchi za Afrika kuwa makini na shule za binafsi ili kuzuia uwezekano wa kuzalisha magaidi kutoka katika shule hizo.

Imedaiwa kuwa magaidi huwekeza katika taasisi mbalimbali za umma zikiwamo shule.

Akizungumza katika kumbukizi ya miaka minne ya kupambana na kundi la kigaidi lililojulikana kwa jina la FETO nchini Uturuki, Balozi mstaafu wa Uturuki nchini, Ali Davutaglu, alisema juzi kuwa magaidi wasipothibitiwa katika nchi, wanaweza kuingia katika ngazi mbalimbali za kiutawala za nchi husika na kuvuruga mipango ya nchi.

"Kwa kuwa Serikali ya Uturuki ilielewa kinachoendelea, hatua stahiki za kisheria zilichukuliwa dhidi ya kundi la kigaidi la FETO na kufunga mfumo wa mawasiliano yao ya siri," alisema Balozi Davutaglu.

Alizitaja njia zilizotumika kupambana na kundi hilo ni kupitia mfumo wa kisheria, na kwamba hatua mbalimbali za kisheria zinaendelea pamoja na kufanyika uchunguzi ili kulimaliza kabisa kundi hilo lililofanya jaribio la mapinduzi mwaka 2016.

Alisema kwa kuwa kundi hilo linajaribu kutumia njia za kisiasa katika kujenga imani kwa wananchi, juhudi mbalimbali zimefanyika katika kudhibiti kuenea kwa kundi hilo kupitia vyombo vya habari na taasisi mbalimbali za umma zikiwamo shule na benki.

Balozi huyo alisema kundi hilo lilianza kwa kampeni kwa wazazi na watoto kuliamini, huku zikitolewa ahadi za maisha mazuri na ajira kwa watoto watakapomaliza kusoma, jambo ambalo balozi huyo alisema lililenga kuwashawishi na kuwatumia kwa malengo ya kundi hilo kinyume cha katiba na sheria za nchi hiyo.

Jaribio hilo la mapinduzi baada ya kushindwa, serikali ya Uturuki iliwakamata maelfu ya watu wakiwamo wanajeshi, watumishi wa umma, wanasiasa na makundi mengine kadhaa.




## Semina yamwamsha anusuru nyumba chupuchupu kuuzwa na mume wake




## Wakulima wanaostaafishwa jembe la mkono, kupitia kampeni ya plau


# BUFE

IJUMAA JULAI 17, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


# UNATEGEMEWA; Project CLEAR, TFF zaungana kuhamasisha usalama mashabiki viwanjani

• Penye mechi; kunawa mikono, kukaa mbali




Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, akifuatiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangwala, kulia ni Mkurugenzi wa Wizara ya Michezo, Hamisi Singo, kwenye kampeni ya kunawa mikono - Unategemewa, katika Uwanja wa Michezo wa Majaliwa, mjini Lindi. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani inaendelea na mapambano ya kudhibiti ugonjwa wa COVID-19. Kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Taifa linaendelea kuchukua hatua mbalimbali kupiga vita ya maradhi hayo, ikiwamo kutoa elimu na kutengeneza programu mbalimbali za ushirikishwaji katika jamii.

Wizara ya Afya kwa ushirikiano na Project CLEAR inatekeleza kampeni ya 'Usichukulie Poa Unategemewa' inayolenga kuhamasisha kila mtu bila kujali umri, kipato, wala nafasi yake katika jamii anashiriki katika kuifanya Tanzania kuwa salama dhidi ya maambukizi ya COVID-19.

Project CLEAR, pia ndio watekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira maarufu kama 'Nyumba ni Choo' kwa niaba ya Wizara ya Afya.

Ili kuhakikisha ujumbe unafika kwa walengwa wengi zaidi 'Project CLEAR' imeingia ubia na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutumia jukwaa la soka kufikisha ujumbe kwa walengwa wengi zaidi ili kubadili tabia.

Ni katika utekelezaji huo, Project CLEAR imeweka vifaa mahsusi vya kunawa mikono katika viwanja 18 vya soka nchini, ambavyo michuano ya Ligi Kuu ya Vodacom nchini (VPL) inaendeshwa kitaifa.



Pamoja vifaa hivyo kubeba ujumbe unaoelimisha jamii kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa wa COVID-19, pia inatoa fursa kwa wachezaji na mashabiki kutumia miundombinu hiyo kunawa mikono kabla ya kuingia uwanjani.

Katika tukio la kuelimisha jamii kupitia kampeni hiyo lililofanyika katika Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi mnamo Julai 8 mwaka huu, wakati wa mechi kati ya timu za Namungo FC na Simba,mgeni rasmi ambaye ni Msemaji wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisisitiza kila mmoja kwa nafasi yake kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa wa COVID-19 katika kipindi hiki ambacho serikali imeruhusu shughuli kuendelea kama kawaida.

Kuhusu COVID-19, Dk. Abbas anasema licha ya hali kutengemaa nchini na shughuli nyingi zilizosimamshwa kurejeshwa, kuna haja ya kuendelea kuzingatia tahadhari za kiafya kama kunawa mikono na kuzingatia tofauti ya umbali kati ya mtu mmoja na mwingine.

Itakumbukwa, baada ya kuripotiwa kuwapo wagonjwa wa COVID-19 nchini, serikali ilichukua hatua ya haraka ikiwamo kusimamisha shughuli za masomo kwa miezi mitatu, huku kukiwapo mengine yaliyoendeshwa nchini kwa masharti, ikiwamo uvaaji barakoa na umbali kati ya mtu mmoja na mwingine.

Akizungumzia juhudi za TFF kuhakikisha usalama katika viwanja vya mpira, Katibu wake, Mkuu Wilfred Kidao, anasisitiza azma ya shirikisho hilo kutekeleza vita dhidi ya COVID-19.

Kidao anasema, wanajali usalama na afya ya kila shabiki kwa kusimamia utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Rai ya Kidao kwa mameneja wa viwanja vya soka, ni kwamba wahakikishe mashabiki wachache wanaoingia uwanjani wanachukua tahadhari zote kama kunawa mikono, kukaa katika umbali wa hatua tatu na kuvaa barakoa inapobidi wakiwa ndani ya viwanja vya michezo.

UCHUMI

# Semina yamwamsha anusuru nyumba chupuchupu kuuzwa na mume wake

## • Kufika nyumbani alianzia ukaguzi nyaraka • Alizinasa mafichoni zimebadilishwa miliki • Hatua? Alimbana akakiri...sheria mbioni

**Na Elizabeth Zaya**



Wanawake wa kikundi cha Sauti ya Jamii wakiwa kwenye semina. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

MWANAMKE kila anapojitosa katika pilika kusaka ajira au huduma nyinginezo, anajikuta kuangukia vikwazo vya kijinsia.

Ni kilio cha aina hiyo kutoka kwa kinamama kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Ukonga jijini Dar es Salaam, 'wakifunguka' katika semina inayohusu namna wamavyotambua haki zao na kuzisimamia.

Miongoni mwa yanayochomoza baada ya kuelimika katika semina, ni suala la rushwa katika maeneo mbalimbali ya ofisi wanapohitaji huduma au ajira.

Lucy Makula, Msaidizi wa Kisheria katika Kata ya Kipunguni, anasema kuombwa rushwa ya ngono ni changamoto kubwa wanayokutana nayo na imeendelea kuwa kikwazo kwa wanawake hata wakashindwa kupata huduma au nafasi za uongozi katika nyanja mbalimbali.

Anasema, hilo limekuwa likiwakatisha tamaa wanawake, pale wanapotafuta haki na huduma katika azma ya kufikia malengo ndani ya nyanja tofauti.

Lucy anafafanua namna wanavyokumbana na malalamiko ya wanawake kuombwa rushwa ya ngono, katika nyendo zao za kusaka ajira katika taasisi mbalimbali na wanapokataa, wanaishia kunyimwa nafasi hizo.

Pia, anataja malalamiko mengine ni baadhi ya wanawake wenye ajira, wanajikuta ama wanafukuzwa kazi au mikataba yao ya ajira kukatishhwa katika mazingira tata, kutokana na madai ya rushwa ngono, inapotokea amegomea ombi.

"Wengine wanaombwa, wanapokwenda kutafuta kazi, wengine wanafukuzwa wakiwa kazini, wanapokataa kutoa rushwa hiyo na wengine hata wanakosa kupatiwa huduma katika taasisi mbalimbali, kwa sababu hiyo," anaeleza Lucy.

Mama huyo anaendelea: "Mfano, hata katika masuala ya kutafuta nafasi ya uongozi, wanawake wanateswa sana na jambo hili. Unakuta anaombwa rushwa ya ngono na kila mtu akiahidiwa kwamba akifanya hivyo atapata nafasi ya uongozi. Hili ni tatizo kubwa na linawakwamisha wengi.

"Sijui kama jambo hili litaisha! Wanawake tumekuwa tukipambana sana, lakini tunarudishwa nyuma na watu wasiotutakia mema. Kuna shuhuda nyingi sana za wanawake au wasichana kuomba rushwa hiyo."

Lucy anasema, kwenye ulingo wa siasa, eneo ambalo kitaifa hivi sasa joto lake liko juu kuelekea uchaguzi hatua kuu sasa ni mchakato wa kupata wagombea kuna matatizo mengi yanayoendana na wanawake kuombwa rushwa ngono.

"Kwenye siasa ndiyo usiseme, huko tena ndiyo hatari. Angalau msichana mwenye umri mdogo anaweza kufikiriwa kupewa nafasi kwa lengo la kwamba aingie ili ndiyo wamuombe vizuri, lakini mwanamke mwenye umri mkubwa zaidi asipotoa hapo hapo hapati kabisa," anasema Lucy.

> **"Mpaka hivi tunavyozungumza, nyaraka zote ninazo. Nimewajulisha wasaidizi wa kisheria na wanapanga kumuita na kumweleza endapo atakuwa mbishi, tutamchukulia hatua nyingine za kisheria.**

Ofisa Ustawi wa Jamii Kata za Msongola na Kivule, Msekwa Joliga, anaunga mkono wamekuwa wakipokea wanawake wengi wanaohitaji kusaidiwa baada ya kuomba rushwa hiyo ya ngono, kutoka taasisi mbalimbali za ajira na zinazotoa huduma.

"Tunapata kesi nyingi ambazo wanawake na wasichana wamekuwa wakija kulalamika, kwamba wanaombwa rushwa ya ngono na viongozi katika nyanja mbalimbali wanapoenda kutafuta huduma au nafasi za uongozi na tumekuwa tukipambana kuyashughulikia na kuwashauri pia," anasema Joliga.

### KUTOMILIKISHWA MALI

Jambo jingine ambalo anasema wanakumbana nalo ni wanawake walio kwenye ndoa kunyimwa na wanaume zao haki ya kuzimiliki.

Anasema, wanawake wengi wamekuwa wakifika ofisini kwao, wakilalamika kwamba hawaomilikishwi mali wanazotafuta na waume zao,badala yake umiliki unaegemea upande mmoja wa mume.

Pia, Joliga analalamika kuwapo baadhi ya wanawake wanaoishia kuwa mashahidi katika umiliki wa mali walizoshiriki kuzitafuta.


Kinamama wakazi wa Kitunda, nje ya Jiji la Dar es Salaam, wakijadili mikakati ya vikwazo vya maendeleo yanayowahusu. **PICHA: MTANDAO**

"Kuna shida kubwa sana katika suala la namna ya kumiliki mali katika familia nyingi na hii inachangia kwa kiwango kikubwa ndoa au baadhi ya familia kusambaratika," anasema Joliga anaendelea:

"Tuna kesi ambazo huwa tunakutana nazo za baadhi ya wanaume kubadilisha umiliki wa mali bila kuwashirikisha wake zao au wanawake wengine wanashiriki katika ushahidi tu wa kununua mali au mauziano, badala ya nao kutambuliwa kama miongoni mwa wamiliki. Hii michezo ni mingi sana."

### MKAZI ASIMULIA

Sheikh Abdi Mahanyu, kutoka eneo la Kipunguni, anaungana na malalamiko kwamba: "Wanawake wengi huwa wana imani kubwa na waume zao na ndiyo maana wakati mwingine huwa hawajishughulishi hata kutaka kujua zinapohifadhiwa nyaraka za mali wanazokuwa wameshirikiana kuzitafuta.

"Sasa kwa baadhi ya wanaume wasio na hofu ya Mungu, wanatumia mwanya huo kama fimbo ya kuwaumiza wake zao kwa kuuza na wakati mwingine kutumia vibaya na kuacha familia kwenye mateso."

Sheikh Mahanyu anashauri wanawake kujenga tabia ya kuwadadisi waume kuhusu nafasi kwenye umiliki wa mali, kwa sababu ya kujilinda katika miliki ya mali walizoshiriki kuzitafuta ziko salama.

"Siyo vizuri unakuta baadhi ya wanawake hawajawahi hata kuuliza zilipo nyaraka za mali, inabidi na wao wajifunze na kufanya hivyo siyo kosa," anashauri Sheikh Mahanyu.

### ALIYESAIDIWA KUAMKA

Mshiriki mafunzo (jina la pili tunalo ), kutoka Kata ya Kipunguni ana ushuhuda kuhusu namna mafunzo yaivyomsaidia, hta akafanikiwa kuokoa nyumba yake iliyokuwa mbioni kuuzwa na mzazi mwenzake.

Anasimulia kwamba hakuwa na wazo la kufuatilia nyaraka za nyumba yake kwa miaka mingi, lakini baadaye aliamka.

"Mimi ni miongoni mwa wanawake ambao semina hii imeniokoa 'chupu chupu.' Mimi ninamiliki nyumba ambayo kwa kiasi kikubwa ilitokana na mchango wangu.

"Mzazi mwenzangu hakuchangia pakubwa, kwa hiyo baada ya semina na tukakumbushwa kukagua nyaraka za umiliki wa mali. Niliporudi nyumbani nilienda moja kwa moja hadi pale nilipokuwa nimehifadhi," anaeleza na kuendeleza simulizi:

"Huwezi kuamini ni kama semina ilikuwa inanilenga mimi. Sikukuta zile nyaraka pale nilipokuwa nimezihifadhi siku nyingi. Nilichanganyikiwa, nilianza kupekua kila sehemu na kwenye vitu vya mzazi mwenzangu na bahati nzuri nikaziona alikuwa amezificha.

"Nilizichukua, lakini cha kushangaza nilikuta na nyaraka nyingine ambazo zilionyesha kuwa alikuwa ameanza mchakato wa kuzibadilisha, hati ya nyumba tulikuwa tumeandika jina la mtoto wetu, lakini alikuwa amebadilisha na kuandika majina yetu mimi na yeye na baadaue nilipomuuliza alisema amefanya hivyo ili aiuze."

Anaeleza hatua aliyochuka, ni kwamba ilimbidi azichukue nyaraka tajwa na kuanza kuchukua hatua ya kuzuia mauzo ya nyumba isiuzwe, kwa sababu walikuwa wamekubaliana mali ni ya watoto wao.

"Mpaka hivi tunavyozungumza, nyaraka zote ninazo. Nimewajulisha wasaidizi wa kisheria na wanapanga kumuita na kumweleza endapo atakuwa mbishi, tutamchukulia hatua nyingine za kisheria," anasema mama huyo.

### MKURUGENZI KIKUNDI


Mkurugenzi wa Sauti ya Jamii katika Kata hiyo ya Kipunguni, Selemani Bishagazi ambaye ni msaidizi wa kisheria katika eneo hilo, anakiri kupatiwa taarifa ya mama huyo na kwamba bado wanasubiri kuzungumza na mume wake.

"Ni kweli huyu mama alikuja kutueleza kwamba mzazi mwenzake anataka kuuza nyumba ambayo walikuwa wamemwandika mtoto wao kama mmiliki. Sisi tunasubiri kuzungumza na mume wake kabla ya kumshauri kuchukua hatua nyinginezo.

"Matukio ya namna hii huku tumekuwa tukikutana nayo mengi sana na mengi huwa tunayamaliza kwa ushauri. Ni machache ambayo hushindikana na kufika mbali katika vyombo vya sheria. Tatizo kubwa la wananchi wengi hawana elimu ya haki za kisheria."

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Waheshimiwa wabunge karibuni mtaani!





**NA JOSEPH KULANGWA**

NIKO katikati ya mji, nakutana na meti wangu wa shule ya msingi, ambaye hivi karibuni alikuwa anapenda nimuite mheshimiwa, kwa sababu tu alikuwa mbunge. Mwakilishi wa wananchi bungeni.

Hakutaka kabisa nimuite vinginevyo na kila nikikosea alinikumbusha na kusisitiza kuwa yeye ni mheshimiwa mbunge na nikimuita vinginevyo, namdhalilisha yeye pamoja na wapiga kura wake.

Lakini leo naona kanyweea, namuita nitakavyo sasa. Kwa sababu si mbunge tena, Rais kishavunja Bunge. Sasa karejea kwetu huku mitaani anaweza kutangaza nia tena.

Anaona shida sana kukaa mtaani bila ya kuitwa mheshimiwa. Mazoea mabaya! Anataka kufa na uheshimiwa wake.

Nami namkaribisha mtaani na kumtakia kila la heri katika mipango yake mingine ya kwenda bungeni, ambako hata hivyo nampa makavu tu, kuwa sikupata kumsikia akichangia hoja hasa zinazohusu kutungwa 'sharia' mpya, hata maswali.

Ni kweli kabisa, zaidi ya kusikia akihanikiza tu ndiyooo! Katika kundi la wenzake na siku ile ya mwisho ya kuhojiwa mmoja mmoja na kujibu ndiyo au hapana.

Nilimsikia siku hiyo akijibu ndiyo. Akikubali Bajeti Kuu ipite. Zaidi ya hapo sikupata kabisa kumsikia.

Si yeye tu, walikuwapo wengi wa aina hiyo. Wabunge ambao hawachangii chochote, wabunge ambao mradi waingie tu mjengoni, kwa kuchaguliwa, kwa kuteuliwa au kwa viti maalumu, ili mradi waonekane wapo na kusaini basi. Wapo wengi na wengine mnawajua.

Wale ambao pia majimboni ndiyo sasa wanafikiria kwenda. Nadhani kujitambulisha upya. Wapo.

Sikutaka kumuacha hivi hivi, nikamhoji sababu za kukaa kimya bungeni bila ya hata ya kuchangia kitu, ananiambia we acha tu!

Sasa wee acha tu ina maana gani? Namng'ang'ania, mpaka anafunguka. Anasema mambo ni mengi na muda hautoshi.

Namkaba koo kwa kumuuliza kwa nini alikuwa anatambia uheshimiwa na gari zuri wakati bungeni hakuwa hata na cha kusema? Anasema, eti bungeni mambo si rahisi kama ninavyodhani. Namshangaa, mambo magumu hata kuuliza swali la maji au barabara?

Namuuliza mbona maswali hayo mi kama yalishatengenezwa tangu miaka ile enzi za Chifu Adam Sapi Mkwawa? Namuuliza ni lini Bunge likae yasiulizwe maswali kama hayo, ya Mheshimiwa Spika katika jimbo langu hatuna maji wala barabara? Ni lini?

Nikamuuliza ni lini naibu waziri aliacha kujibu kwa niaba ya waziri, kuwa swali hilo ni zuri na ni la kweli na sasa wamo katika mkakati na mpango endelevu wa kuhakikisha kabla Bunge hili halijamalizika mimi na Mheshimiwa Mbunge tutakwemda eneo la tukio kujionea hali halisi na kuifanyia kazi. Ni lini?

Nikamwambia, kwani sijui kwamba hata kama angeuliza swali la nyongeza angepaswa kusema kuwa pamoja na jibu au majibu mazuri ya Naibu Waziri au Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza, kwamba ni kwa kiasi gani tatizo hilo litashughulikiwa!

Na baada ya hapo kwani sijui kwamba Naibu Waziri au Waziri atajibu kwamba anawapongeza waliokuchagua kwa sababu umekuwa ukifuatilia matatizo ya wananchi wako na hata kabla ya kuingia kwenye kikao husika mlizungumza?

Na hapo ndipo nawe utaridhika, kwa sababu tayari umetimiza kilichokupeleka bungeni?

Ananiacha hoi kwa kuniambia kuwa hata hivyo Bunge halikuwa mbashara a.k.a laivu, sasa kulikuwa na maana gani kupoteza muda kupiga kelele wakati wapiga kura hawakuoni?

Akataka kunishinda pointi hapo, lakini nami nikamuwahi, kwani mbashara ndio unaomaliza matatizo ya wananchi jimboni?

Akidhani amenishinda, akasema hivi unajua maana ya siasa na wanasiasa? Usiposikika nani atakujua? Usipoonekaa kwenye luninga nani atakutambua? Ilikuwa kidogo nianze kumuelewa.

Mara nikamsikia Spika Job Ndugai akihojiwa mahali akisema, mbunge ukimwachia wasaa kidogo tu kwenye luninga akaonekana...na wengine wakiandaa wapiga kura kuwa mtaniona leo luningani, umekwisha.

Akasema, atasema huyo, atatukana huyo, ili mradi asikike tu ameikosoa serikali na tena kwa kutukana. Nikamuuliza umemsikia Ndugai? Akanijibu eti ndiyo zake huyo. Sasa mimi naweza kutukana serikali ya chama changu? Labda hao wenzetu. Lakini nao mbona wanahamia huku? Haraka sijui imetoka wapi, akaniaga. Alamsiki.

**Simu: +255 713 410008 na barua pepe:jkulangwa@yahoo.com**

UCHUMI

# Wakulima wanaostaafishwa jembe la mkono, kupitia kampeni ya plau

• Staili ya kuwafikishia vikundi rafiki



Wakulima wakitumia jembe la kukokotwa na ng'ombe. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

WAKULIMA wengi nchini wanaangukia kundi la wakulima wadogo na maisha yako vijijini, wakiwa ndani ya sekta inayoajiri zaidi ya theluthi tatu ya Watanzania na inalisha wastani wa Watanzania milioni 50.

Katika kukifanikisha kilimo hicho, wanatumia zana duni hasa, jembe la mkono ambalo leo hii linatajwa kupitwa na wakati.

Mbali na walakini wa kuegemea jembe la mkono, kuna la pili kwamba ukuzaji mazao shambani, tegemeo lake kuu ni kuegemea msimu wa mvua na kuna wakati wakulima hujikuta wakipata mavuno kidogo, kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Kampeni mbalimbali zimekuwa zikifanyika kwa lengo la kuwasaidia wakulima, angalau wapate unafuu kwenye shughuli zao za kilimo hicho cha kutumia jembe la mkono na msimu wa mvua.

Ndani ya kampeni za awali, ni kuvisaidia vikundi vya wakulima majembe ya kukokotwa na ng'ombe - plau, ili kuviwezesha kulima maeneo makubwa, badala ya kutumia jembe la mkono ambalo halina uwezo.

Vikundi vya wakulima wa Musoma Vijijini mkoani Mara, ni miongoni mwa waliofaidika na msaada wa majembe hayo na ulioanza kutolewa tangu Desemba mwaka jana na bado unaendelea kutolewa.

**NAMNA ILIVYO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, John Kayombo, anasema kuna mdau wa maendeleo aliyeibua kampeni ili kuhamasisha wakulima kuachana na jembe la mkono, huku akigawa plau kwa vikundi vya wakulima.

> “Wakulima wamehamasishwa kujikita kwenye kilimo cha mazao ya chakula na biashara, badala ya kutegemea uvuvi tu, ambao kwa sasa una changamoto nyingi, ikiwamo ukosefu samaki.



Baadhi ya vikundi vya wakulima wakiwa na majembe yao ya kilimo waliokabidhiwa.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, anasema alianza programu hiyo Desemba mwaka jana, kwa kutoa plau 20 na kisha kwenye Aprili mwaka huu, akagawa plau nyingine 25.

Mkurugenzi huyo anafafanua: “Baada ya hapo, wakati wa sikukuu ya Iddi, aligawa majembe mengine 40 kwa vikundi vya wakulima na sasa anajiandaa kutoa mengine 50 wakati wa Sikukuu ya Wakulima (Nanenane).”

Kayombo anasema, majembe ambayo hadi sasa ameshatoa yanazidi idadi ya vijiji vilivyopo ambavyo ni 68. Kinachofanyika ni kwamba zana hizo zinaelekezwa kwenye vikundi vya wakulima, vijiji vingi vikiwa na wastani wa vikundi kati ya kimoja hadi vitatu.

“Wadau wa kilimo wameamua kusaidiana na serikali katika kuwakomboa wakulima kutoka kwenye kilimo cha kujikimu na ndiyo maana wameanza na plau hii kwetu ni hatua nzuri,” anasema Kayombo.

Anasema, wakulima wamehamasishwa kujikita kwenye kilimo cha mazao ya chakula na biashara, badala ya kutegemea uvuvi tu, ambao kwa sasa una changamoto nyingi, ikiwamo ukosefu samaki.

Baadhi ya mazao ambayo kwa sasa yanalimwa kwa wingi Musoma Vijijini, ni mihogo, mtama, maharage, viazi vitamu, mahindi, mpunga, alizeti, dengu, mbaazi na ufuta, huku kukiwapo viwanda viwili vya kukamua mafuta ya alizeti.

**USHIRIKISHWAJI**

Kaimu Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Musoma, Ismail Masogo, anatamka kuunga mkono juhudi hizo za kumwondoa mkulima kwenye kilimo cha kijikimu na kupitia hatua kwenda mbele.

“Ofisi yangu ina jukumu la kufuatilia na kutoa maelekezo kwa maofisa kilimo wa kata, kwa ajili ya kusimamia na kuwapa wakulima elimu kuhusu utayarishaji wa mashamba, upandaji, upaliliaji na utunzaji wa mazao,” anasema Masogo.

Wataalamu wa kilimo wana kawaida kuwatembelea wakulima kila mara, ili kuona changamoto zinazowakabili na kuzitatua kwa lengo la kuongeza mavuno na ubora wa mazao mbalimbali.

“Juhudi za kuboresha kilimo zinazofanywa na wadau mbalimbali ni za kuunga mkono, kwani zitaongeza uzalishaji na kuongeza pato la mtu mmoja mmoja huku serikali nayo ikipata kodi,” anasema.

**VIKUNDI VINASEMAJE?**

Mkulima wa Kijiji cha Lyasembe, ambaye ni Mwenyekiti wa Kikundi cha Wakulima wa Mahindi na Dengu cha Kilimo Kwanza, Manyama Makuyu, anasema kilimo cha kutumia plau kinaweza kuwa cha zamani, lakini kina unafuu kuliko jembe la mkono.

“Plau ni ya muda wa mrefu, lakini inasaidia kulima eneo kubwa la shamba kuliko jembe la mkono, hivyo kupata msaada wa plau ni dalili kwamba tunaelekea kwenye trekta hapo baadaye,” anasema Makuyu.

Makuyu anasema, mbali na jembe la mkono, kuna haja pia ya kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua ambazo sasa zinanyesha bila ya mpangilio, kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Kadogo Mashauri, mkazi wa kijiji cha Chirorwe, anasema, utumiaji jembe la kukokotwa na ng'ombe, unaongeza ufanisi kwenye kilimo, hivyo ni jambo linalopaswa kuendelee kuhamasishwa.

“Mimi ninaamini, plau inaweza kukuza kilimo kama wadau wote wataweka msukumo wa kuhamasisha wakulima kuitumia, kwa kuzingatia kwamba bado hatujafikia kuwa na uwezo wa kila mmoja kuwa trekta,” anasema Mashauri.

Anasema, teknolojia ya kulima kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe ni zaidi kuliko jembe la mkono, hivyo kizidi kuhamasishwa huku wakipewa zana hizo bure ili waendelee kuboresha kilimo chao.



# Uboreshaji huduma za afya ulivyopunguza vifo vya uzazi

**Na Augusta Njoji,** BAHI

UBORESHAJI wa huduma za afya uliofanywa na serikali katika Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, umepunguza vifo vya mama na mtoto kutoka vinane mwaka 2015/16 hadi kimoja mwaka 2019/20.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mwanahamisi Munkunda, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uboreshaji wa huduma za afya wilayani huko.

Alisema uboreshaji huo umechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya uzazi na hicho kifo kimoja ni agharabu kutokea.

"Inaweza kutokea kutokana na sababu ambazo wakati mwingine ni nje ya uwezo au matakwa ya Mwenyezi Mungu, lakini kwa kitabibu kwa kweli tumeongeza ufanisi mkubwa, vituo vyote ambavyo vimekarabatiwa vina huduma ya upasuaji," alisema.

Akizungumzia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Fatuma Mganga, alisema utagharimu Sh. bilioni mbili hadi kukamilika kwake na sasa umefikia asilimia 98.

"Hizi asilimia mbili zilizobaki ni pamoja na ufungaji wa mfumo wa TEHAMA, na hii inatokana na agizo la serikali kwa hospitali zote kutumia mfumo wa TEHAMA kwenye makusanyo yake, na tayari umefungwa na umefikia asilimia 90," alisema.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Philipina Philipo, alisema hospitali hiyo imeshaanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje ikiwamo huduma za maabara.



Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai (kulia), akizungumza na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), nchini, Christine Musisi, alipomtembelea ofisini kwake, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Tume yaungana na TAKUKURU kuimarisha maendeleo ushirika

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TUME ya Maendeleo Ushirika Tanzania (TCDC), imesema itaendelea kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ili kuimarisha usimamizi na maendeleo ya vyama vya ushirika nchini.

Taasisi hizo zilifanya kikao cha pamoja jana katika makao makuu ya tume hiyo jijini hapa, ujumbe wa TAKUKURU ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Brigedia Jenerali John Mbungo, huku ujumbe wa TCDC ukiongozwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dk. Benson Ndiege.

Akizungumza katika kikao hicho, Dk. Ndiege alisema kazi iliyofanywa na TAKUKURU katika urejeshaji wa fedha kwenye vyama vya ushirika zilizokuwa zimechukuliwa bila kufuata utaratibu, imetoa ujumbe mahsusi kuwa fedha na mali za ushirika hazitakiwi kuchezewa.

"Tutaendelea kushirikiana na TAKUKURU katika kuhakikisha mali za wanachama wa vyama vya ushirika zinalindwa na kuwanufaisha wananchi.

"Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa na Maofisa Ushirika wa Wilaya waendelee kushirikiana na maofisa wa TAKUKURU katika maeneo yao, ili kulinda mali za wanaushirika," alisema Dk. Ndiege.

Alisema taasisi hizo kwa pamoja zina wajibu katika kuimarisha usimamizi na maendeleo ya vyama vya ushirika nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Mbungo, aliwasilisha taarifa ya uchunguzi na fedha zilizokusanywa na taasisi hiyo kwa niaba ya vyama vya ushirika nchi nzima baada ya kukabidhiwa kazi hiyo na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga.

Alipongeza ushirikiano uliotolewa na tume kwa TAKUKURU wakati wakitekeleza maagizo ya viongozi wa serikali katika urejeshaji wa fedha kwenye vyama vya ushirika zilizokuwa zimechukuliwa bila kufuata utaratibu.

"Tuleteeni matatizo na dosari zinazohusu ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya watu wanaoviibia vyama vya ushirika ili tushughulike nao na kuhakikisha kuwa mali za wanaushirika zinakuwa salama," alisema Brigedia Mbungo.

Wajumbe wa kikao hicho walijadili mfumo na utaratibu unaotumiwa na TAKUKURU katika urejeshaji wa fedha zilizokusanywa kwenye vyama vya ushirika na kuangalia njia na mbinu za kuzuia mianya ya wizi na ubadhirifu katika vyama hivyo.

Vilevile, TAKUKURU na TCDC walikubaliana maeneo ya kushirikiana kati ya taasisi hizo mbili.

## CHF wafuatilia wanachama kukosa dawa

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

MRATIBU wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) Jiji la Dodoma, Patrick Sebyiga, amesema wanashughulikia kero zinazowakabili wanachama wao ikiwamo malalamiko ya kukosa dawa.

Sebya aliiambia Nipashe jijini hapa jana kuwa miongoni mwa kero zinazowasilishwa na wanachama wao, hasa wa maeneo ya vijijini pindi wanapokwenda kupata matibabu hospitalini kuambiwa hakuna dawa, lakini anayelipia matibabu kwa fedha taslimu anapata dawa.

"Hii ni dosari ambayo tumeanza kuifanyia kazi, ili tuone ni kwanini wanaambiwa hivyo. Lakini wanachama nao inabidi waelewe kuwa dawa hupelekwa katika hospitali kwa awamu kila baada ya miezi mitatu, sasa inawezekana mtu akaenda zile dakika za mwisho," Sebyiga alisema.

Alitoa wito kwa wakazi wa Mkoa wa Dodoma kujiunga na mfuko huo, ili kuwa na uhakika wa matibabu na kupata huduma za matibabu kwa gharama nafuu.

Alisema wameona ni vyema kila mwananchi akajiunga na bima hiyo, ili kuwa na uhakika wa matibabu, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya serikali ya kila mwananchi kuwa na bima ya afya.

"Serikali imeweka utaratibu kwa wale ambao hawako katika mfumo rasmi, kwa wafanyabiashara wadogo ambao ni mama lishe, waendesha bodaboda na wanafunzi, wakiwa na bima hii ya afya, inawasaidia sana," alisema.

Sebyiga aliongeza kuwa mwamko ni mkubwa na watu wameanza kuwa na uelewa mkubwa kuhusu bima hiyo, akibainisha kuwa wengi wamejitokeza kujiandikisha.

"Sasa hivi mtu anapopata matatizo ya kiafya mfano kuugua, asipokuwa na kadi ya CHF, anaingia gharama kubwa, lakini ukiangalia kiwango ambacho serikali imeweka cha Sh. 30,000 kwa watu sita, hii ni wastani kuwa mtu anatibiwa kwa Sh. 5,000 kwa mwaka," alisema.

Mfuko huo ulioanzishwa kwa Sheria Na. 1 Mwaka 2001 (Sura ya 409) inayotaka kaya, kikundi, familia au mtu binafsi kuchangia gharama za matibabu kabla ya kuugua.



# Mchango wa wadau wa kilimo watambuliwa uchumi wa kati

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imesema inatambua mchango wa wadau binafsi katika kukuza na kuendeleza sekta ya kilimo nchini na kuwa sehemu ya mchango wa kuiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alipoitembelea kampuni ya uuzaji wa zana za Kilimo ya Agricom Africa Ltd iliyopo Kata ya Igurusi, Wlaya ya Mbarali mkoani Mbeya. Kusaya alisema kampuni hiyo imekuwa na mchango mkubwa katika kuwawezesha wakulima nyenzo za kilimo yakiwamo matrekta, pawatila na mashine zinazotumika kuvuna mpunga pamoja na kutoa elimu ya kufanya kilimo bora na chenye tija.

Alisema kwa kuwa sekta ya kilimo ndiyo inayoongoza kwa kutoa ajira nchini, hivyo imekuwa sehemu ya kuchangia pato la taifa nchini kutokana na rasilimali zinazozalishwa kutumika kwa ajili ya shughuli za biashara pamoja na kilimo.

Kwa mujibu wa Kusaya, serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya kilimo nchini kwa kuwa wamekuwa na msaada mkubwa katika kutengeneza mnyororo wa thamani kuanzia kwenye uzalishaji hadi sokoni.

"Mara nyingi ninapopita huwa ninawaona kando ya barababara na nilikuwa nina hamu nije kuona na kujifunza shughuli zenu, kwa kweli nimeridhishwa namna Agricom mnavyofanya shughuli zenu za kuwainua wakulima ili wanufaike na shughuli za kilimo," alisema.

Hata hivyo, alisema hakufanya kilimo cha mazoea ambacho hakina faida na kubadili mwenendo wa kulima kisasa kwa lengo la kupata faida.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Masoko na Mauzo wa Kampuni ya Agricom Africa Ltd, Remmy Nindi, alisema kampuni hiyo imejipanga kuhakikisha inafungua matawi sehemu mbalimbali ili kuwafikia wananchi wengi zaidi. Alisema uwapo wa kampuni hiyo umekuwa ni fursa kwa wakazi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa kuwa wakulima wengi wa kanda hiyo wamenufaika kupitia huduma zinazotolewa na kampuni hiyo.

"Natoa wito kwa wakulima kuendelea kutumia huduma zetu, kwani watu wengi wameweza kunufaika kupitia kilimo cha kisasa ambacho kinachagizwa na zana bora za kilimo kutoka kampuni ya Agricom Africa Ltd," alisema.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo ya matumizi ya baadhi ya zana za kilimo zinazouzwa na Kampuni ya Agricom Africa Ltd, katika Kata ya Igurusi, wilayani Mbarali, alipofanya ziara ya kikazi, mkoani Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kasoro 4 ujazaji fomu za maadili zaanikwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Mbeya imeainisha kasoro nne ambazo hujitokeza mara kwa mara kwenye ujazaji wa fomu za tamko la mali na madeni ya viongozi wa umma na hatua ambazo huwa zinachukuliwa kurekebisha kasoro hizo.

Akizungumza na Nipashe juzi, Ofisa wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Majid Mohamed, alisema moja kati ya kasoro hizo ni viongozi kujaza fomu na kuziwasilisha bila kuwa na mhuri wa kamishna wa viapo.

Alisema kwa mujibu wa sheria, lazima kila kiongozi anayejaza fomu hizo aziwasilishe kwa kamishna huyo ili kuthibitisha kuwa taarifa zilizoandikwa ni sahihi.

Alisema kosa lingine ambalo huwa linajitokeza ni wahusika kutokuweka namba za akaunti za benki ambazo wamehifadhi fedha zao, ili kuiwezesha sekretarieti hiyo kuhakiki kilichoandikwa kwenye fomu na uhalisia wa fedha zilizoko benki.

Vilevile, alisema baadhi ya viongozi wanajaza fomu hizo na kuziwasilisha bila kutaja fedha taslimu ambazo wanamiliki kwenye akaunti zao za benki.

Alisema kosa la nne kwamba ni baadhi ya viongozi kutojaza mali za mke au mume wakati kwenye maelezo binafsi wanakuwa wameeleza kwamba wameoa ama wameolewa na kwamba huwa inaleta tatizo kwenye uhakiki.

"Sheria ya maadili ya viongozi wa umma imetamka kwenye kifungu cha 15 kuwa, kiongozi wa umma atahesabiwa kuwa amekiuka maadili ya uongozi ikiwa atachelewa, atashindwa kwa makusudi kutoa tamko la rasilimali na madeni ama kutoa tamko la uongo," alisema Mohamed.

Alisema kwa kiongozi yeyote ambaye atakiuka taratibu za utoaji wa matamko ya raslimali na madeni, atachukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ambazo zimeainishwa kwenye kifungu cha nane cha sheria ya maadili ya viongozi wa umma.

Alisema baadhi ya viongozi huwa wanataja mali zao kwa usahihi, lakini hawaainishi vyanzo vya mapato yao na kwamba baadhi hutaja mali zenye thamani tofauti kila mwaka jambo ambalo huwa linaleta mkanganyiko wakati wa uhakiki.

Mohamed aliainisha baadhi ya adhabu ambazo kiongozi anayekiuka anachukuliwa kuwa ni kuonywa au kupewa tahadhari, kushushwa cheo, kusimamishwa kazi, kufukuzwa kazi, kiongozi kushauriwa kujiuzuru na kupewa adhabu nyingine kwa mujibu wa taratibu za nidhamu za wadhifa.

Alisema wanaendelea na utaratibu wa kutoa elimu kwa viongozi ili wajaze fomu hizo kwa umakini na kuyaepuka makosa hayo ambayo yanaweza yakawagharimu kwenye kazi zao.

## Wakulima wa pareto waiangukia serikali elimu kudhibiti sumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima wa pareto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuwapatia elimu itakayowasaidia kuzalisha mazao yenye sumu nyingi na inayohitajika kwenye soko.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi hao walisema mara nyingi wanunuzi wa zao hilo wamekuwa wakichukua mazao yao na kwenda kupima kiwango cha sumu kwenye maarara ambazo hawana uwakilishi wowote na malipo wanayoletewa huwa ni kidogo kwa kisingizio kuwa kiwango cha sumu kiko chini.

Mmoja wa wakulima wa Kata ya Iyunga Mapinduzi, Jailosi Shila, alisema hawajawahi kupewa elimu na serikali juu ya njia bora za uzalishaji wa zao hilo ambazo zitawawezesha kuzalisha mazao yenye sumu nyingi kuliko wanayozalisha kwa sasa.

Alisema mara nyingi huwa wanapata elimu kutoka kwa wanunuzi na kwamba wakati mwingine huwa wanashindwa kuiamini elimu wanayopewa kwa sababu wanunuzi hao huwa wanawapunja kwenye malipo kwa kisingizio cha sumu.

"Tunaomba serikali itusaidie wataalamu wa kutupa elimu ya uzalishaji bora wa pareto, kwa sasa tunatumia uzoefu tu na pengine tungepata wataalamu tungefaidika zaidi na zao hili kiuchumi," alisema Shila.


Alisema mnunuzi mkuu wa pareto katika wilaya hiyo huwa anaenda nazo Mufindi mkoani Iringa ambako ndiko kwenye maabara ya kupimia kiwango cha sumu.

Naye Sophia Mwazembe, alisema bei wanayouzia zao hilo kwa sasa ni ndogo ikilinganishwa na gharama wanazotumia kwenye uzalishaji hali ambayo inawafanya baadhi kuanza kukata tamaa ya kuendelea kuzalisha.

Alisema kwa sasa wanauza zao hilo kwa Sh. 2,400 kwa kilo tofauti na maeneo mengine yanayozalisha zao hilo duniani ikiwamo nchi jirani ya Kenya ambayo alidai bei huwa inafika mpaka Sh. 5,000.

"Kuna baadhi ya wenzetu wameng'oa miche ya pareto kwenye mashamba yao na wameanza kupanda miti na wengine wanaamua kulima mazao ya chakula kama mahindi na maharage," alisema Sophia.

Alisema kuna kipindi waliaminishwa na viongozi wa kisiasa kuwa wataletewa kiwanda cha kuchakata zao hilo katika ukanda huo, lakini mpaka sasa dalili hazionekani hali ambayo inawafanya waendelee kutegemea mnunuzi mmoja.



HABARI ZANZIBAR

# Waliokosa uteuzi wa kugombea urais wajitosa ubunge, uwakilishi

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

BAADHI ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliotia nia kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar, lakini hawakubahatika kupata nafasi hiyo, wameamua kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya uwakilishi na ubunge majimboni.

Miongoni mwa wagombea hao ni Dk. Khalid Salum Mohammed amechukua fomu ya kugombea uwakilishi Jimbo la Donge Mkoa wa Kaskazini Unguja kupitia CCM.

Mgombea huyo alisema amechukua uamuzi huo ili kuendelea kuwapatia maendeleo wananchi wa jimbo hilo. Dk. Khalid ambaye aliingia katika kinyang'anyiro cha urais na kufika nafasi ya wagombea watatu walioteuliwa na Kamati Kuu ya CCM, anagombea Jimbo la Donge kwa kipindi cha pili.

Mwingine ambaye aligombea nafasi ya urais wa Zanzibar, lakini hakufanikiwa ni Rashid Ali Juma, ambaye amechukua fomu kuwania nafasi ya uwakilishi Jimbo la Amani Mjini Unguja.

"Nimechukua fomu ya kuwania nafasi ya uwakilishi katika Jimbo la Amani kwa ajili ya kuendeleza mambo mazuri ambayo niliyasimamia katika kipindi cha miaka mitano iliyopita," alisema Juma.

Mwingine ni Mmanga Mjengo Mjawiri, ambaye amechukua fomu kwa nafasi ya uwakilishi katika Jimbo la Mkoani baada ya kukosa kuteuliwa nafasi ya urais ambayo aligombea.

Mjawiri ambaye ni Waziri wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi, alieleza kuwa endapo atapata nafasi hiyo, kitakua ni kipindi chake cha miaka kumi kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Mkoani Pemba. Kadhalika, yumo aliyegombea nafasi ya urais wa Zanzibar na kuingia katika tano bora, Profesa Makame Mbarawa, ambaye amechukua fomu kuwania nafasi ya ubunge Jimbo la Mkoani Pemba.



Kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Sada Mkuya (kulia), akichukua fomu ya kuomba ridhaa ya kugombea uwakilishi, Jimbo la Kikwajuni, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanawake wenye ulemavu waitwa kugombea

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAKATI harakati za uchukuaji wa fomu za kugombea nafasi mbalimbali za uongozi majimboni katika vyama vya siasa zikiendelea, watu wenye ulemavu wametakiwa kugombea nafasi ya uongozi ili kutimiza haki yao ya kidemokrasia.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wenye ulemavu, Salma Saadat, wakati akizungumza na Nipashe Mjini Zanzibar.

Alisema wimbi kubwa la vijana na wanawake wamehamasika kuchukua fomu za kugombea nafasi za uongozi kupitia vyama vyao vya siasa, lakini ushiriki wa watu wenye ulemavu bado haujaonekana.

Alisema kuwa nafasi hizo za uongozi ukiwamo ubunge, uwakilishi na udiwani kila mwenye sifa ana haki ya kugombea bila ya kujali hali yake ya kimaumbile.

"Watu wenye ulemavu na wao wana haki ya kuwa viongozi isiwe wao kazi yao kuchagua tu wakati na wao wanapaswa kuchaguliwa, hivyo nendeni mkachukue fomu msiogope," alisema.

Alieleza kuwa vyama vingi vya siasa vimeshakamilisha zoezi la uchukuaji wa fomu kwa nafasi ya urais wa Zanzibar, lakini hakuna mtu mwenye ulemavu aliyejitokeza kugombea nafasi hiyo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wasioona Zanzibar, Fatma Jaa, alisema kuwa uwezo mdogo wa kifedha walionao watu wenye ulemavu ni moja ya kikwazo kinachowakabili hasa katika kugombea nafasi za uongozi.

Alisema kuwa nafasi za uongozi katika siasa zinahitaji gharama ya kifedha ikiwamo gharama za uchukuaji wa fomu na mambo mengine na watu wengi wenye ulemavu uwezo wao wa kifedha ni mdogo.

# Katibu muhtasi wa waziri aingia mbio kuwania ubunge wa Jimbo Bububu

Na Rahima Suleiman,
ZANZIBAR

KATIBU Muhtasi wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Fatma Adam Salim, amejitokeza kuomba ridhaa ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kumchagua kuwa mgombea wa ubunge Jimbo la Bububu katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Fatma alikabidhiwa fomu ya kuwania wadhifa huo na Kaimu Katibu wa Wilaya ya Mfenesini, Asha Mzee Omar, baada ya kupokea maombi ya kumtaka kugombea nafasi hiyo kutoka kwa baadhi ya wazee na vijana katika jimbo hilo. Fatma alisema iwapo wanachama watampatia ridhaa ya kuwa mgombea wa ubunge katika jimbo hilo na kuchaguliwa na wananchi, atahakikisha anatumia juhudi na maarifa yake kuwaletea maendeleo wananchi kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Baada ya kutafakari kwa muda mrefu maombi ya wanachama wenzangu wakiwamo wazee na vijana, nimeamua kujitokeza kuchukua fomu ya kuomba ridhaa wanachama kunichague kugombea ubunge Jimbo la Bububu," alisema Fatma.

Alisema pia ameamua kugombea jimboni ili kuhakikisha uwakilishi wa wanawake katika vyombo vya kutunga sheria wa 50 kwa 50 unafikiwa badala ya kutegemea nafasi za viti maalum kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba.

Alisema wanawake wameonyesha uwezo na wanapaswa kujitokeza kugombea katika nafasi za majimbo ili kuhakikisha uwiano unapatikana katika nafasi za uongozi kati ya wanawake na wanaume Visiwani Zanzibar.

Aidha, alisema juhudi za kuwaletea maendeleo zinazofanywa na Rais John Magufuli na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein pia zimemsukuma kugombea wadhifa huo ili kuchangia nguvu zake katika kuongeza kasi ya maendeleo.

Idadi ya wanawake wanaojitokeza kugombea nafasi za ubunge na uwakilishi majimboni inazidi kuongezeka Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;187/2020**

Ombi la SIA LIBORIAS NGAO,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ROLLAND ANTHONY NAKAME. Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 16/07/2020.

158147

## KUPOTEA KWA VYETI



**SEDRICK KANTABULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P1474-0107 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia WHITE LAKE SEKONDARY SCHOOL CENTRE mwaka 2010. Basic Technician Certificate in Accountancy chenye namba TIA/MBY/BTCA/2011/2012/112 kilichotolewa na TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY mwaka 2012. Diploma Certificate in Accountancy chenye namba MBY/DA/12/03201 kilichotolewa na TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY mwaka 2014.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/CEN/RB/160048/2020.**

158141

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**KTK MAHAKAMA YA TEMEKE**
**WILAYA YA TEMEKE**
**MIRATHI NA: 40/2020**

Maombi ya barua za usimamizi wa mirathi ya marehemu:
PENDO EPHRAIM AROKO.
NA
Muombaji: GILLEAD OKY AROKO

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**( Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu iliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa udhibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya Tarehe 06 mwezi 08 mwaka 2020.

Imewasilishwa Leo Tarehe 14 mwezi 07 mwaka 2020.

158150

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ANET MWAMBOSA KIPOMEZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 396 DEN aina ya Toyota Haice Commuter.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.**

Taarifa ya polisi
MBE/MBE/RB/530266/2020.

158152

## FOR SALE

**The Royal Embassy of Saudi Arabia** Dar es Salaam is able to sale the conference equipment as follows:-

- Big Screen TV
- UPS
- Camera
- 11 pcs of microphone
- Speakers
- Sequence power switch
- Conference system control unit
- Camera and multimedia controller

**Contact:**
**+255 22 266 7833 /**
**+255 22 266 8203**
**Email: tzemb@mofa.gov.sa**

158149

## MNADA WA HADHARA

**PSALM AUCTION MART LIMITED,** Kwa idhini tuliopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LIMITED,** tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba/ viwanja kama jedwali linavyoonesha hapa chini. Muda wa mnada ni kuanzia **SAA NNE ASUBUHI**

| MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| Saidi Hamisi Kabange | Nyumba | Pugu Station | 03/08/2020 |
| Ally Amir Kasongo | Kiwanja Chenye Msingi | Chamazi - Msufini | 31/07/2020 |
| Sarafina Rafael Msengi | Nyumba | Majohe Mtaa Wa Rada | 26/07/2020 |
| Faisal Said Mohamed | Nyumba | Majohe Mtaa Wa Rada | 26/07/2020 |
| Omar Bakari Wachopa | Nyumba | Mkuranga Mlamleni-Churwi | 01/08/2020 |

**MASHARTI YA MNADA**
Mnunuzi atalipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa salio halirudi na mnada kurudiwa tena. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi

**MAWASILIANO: PSALM Auction Mart: 0674821287 /0787785659**


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI**

**INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB:**

**+255 - 0782253676**






TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI PICHA



Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (kulia,) akipokea fomu ya kuomba kuwania tena ubunge wa jimbo hilo, mkoani Mara, kutoka kwa katibu wa chama hicho, Wilaya ya Musoma Vijijini, Peter Mashenji, juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**



Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mkoa wa Kilimanjaro, Grace Kiwelu, akipita mbele ya wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho, Jimbo la Vunjo, juzi kuomba ridhaa ya kugombea ubunge katika jimbo hilo, ambapo aliibuka mshindi kwa kupata kura 80 kati ya 84 zilizopigwa. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**



Wagombea wa nafasi ya ubunge, Jimbo la Moshi Vijijini, kupitia Chama cha Demokrasia (CHADEMA), Lucy Ndesamburo (kulia), Sisty Massawe (katikati) na Emanuel Nyaki, wakisubiria matokeo wakati wa uchaguzi wa kura za maoni uliofanyika katika eneo la Garden, kutoka kulia ni Lucy ambaye aliibuka na ushindi wa kura 129 kati ya 137 zilizopigwa. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**



Mwandishi wa Habari, Shadia Suleiman (kushoto), akichukua fomu ya kugombea udiwani wadi ya Mwera Mtofaani kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**



Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Vrajilal Jituson (kushoto), akichukua fomu kutoka kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Babati Vijijini, Filbert Mdaki, kwa ajili ya kuomba kutetea nafasi hiyo, jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Rufiji, Omary Mtua (kushoto), akimkabidhi stakabadhi ya malipo ya fomu ya ubunge, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Rufiji, Mohammed Mchengerwa anayewania tena nafasi hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# SOLSKJAER ALALAMIKIA UPENDELEO KWA CHELSEA




**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema "sio sawa" Chelsea kupewa saa 48 zaidi za mapumziko kuelekea mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA utakaochezwa Jumapili.

United watacheza na wapinzani wao hao Chelsea katika dimba la Wembley ili kutafuta nafasi ya kutinga fainali, na wao kuachwa wacheze mchezo wao wa jana Alhamisi wa Ligi Kuu England dhidi ya Crystal Palace.

Chelsea wataingia kwenye mchezo huo bila kucheza tangu Jumanne na Solskjaer alihoji hilo wakati United pia wakijaribu kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kuna jambo, kwa uhakika kabisa, na hivyo walipewa saa 48 za kupumzika na kuwa na wakati mzuri kuliko sisi," amesema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Sio sawa. Tunazungumza kuhusu usawa kwa ratiba inayopangwa na wenzetu wamepewa muda wa kupumzika, hii sio sawa kabisa.

"Lakini mimi nililazimika kufikiria kuhusu mchezo wa jana Alhamisi (dhidi ya Crystal Palace), na hilo linatufanya sisi kuwa kwenye wakati mgumu."

United waliingia jana kucheza dhidi ya Palace wakiwa hawajapoteza mchezo wowote kati ya 18 katika mashindano baada ya Jumatatu kutoka sare ya kufungana mabao 2-2 dhidi ya Southampton.

# Arteta: Tutasajili wachezaji wapya

**LONDON,** England

ARSENAL kwa uhakika kabisa wanahitaji kusaini wachezaji wapya kwenye soko la usajili licha ya kuifunga Liverpool, kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Mikel Arteta.

Arteta na Arsenal walikuwa na muda mzuri wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Liverpool kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumatano.

Arsenal walianza kuwa nyuma kwa bao la Sadio Mane, lakini walisawazisha kupitia Alexandre Lacazette kabla ya Reiss Nelson kufunga la ushindi.

Licha ya ushindi huo wa kushangaza, Arsenal wapo nafasi ya tisa kwenye msimamo wakiwa wamebakiwa na mechi mbili ligi kumalizika – wakipitwa pointi 40 na vinara Liverpool na Arteta alisisitiza washikabunduki hao wanatakiwa kujiimarisha.

"Nafikiri kwa uhakika kabisa tunahitaji kuimarisha kikosi chetu" alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

Tangu mwaka 2004 Arsenal haijashinda taji la Ligi Kuu England, wakishindwa kumaliza kwenye nne bora tangu walipomaliza nafasi ya pili msimu wa 2015/16.

Tofauti hiyo imeendelea kuwa kubwa kwenye Ligi Kuu, huku Arsenal – ambao walimfukuza Unai Emery Novemba, mwaka jana wamepitwa pointi sita kumaliza kwenye nne bora.





# Berbatov aamua 'kumpasha' Bale

**MADRID,** Hispania

DIMITAR Berbatov amemjia juu nyota wa Real Madrid, Gareth Bale kwa "tabia yake ya utovu wa nidhamu na kutoonyesha heshima" kwa miamba hao kutoka mji Mkuu wa Hispania.

Bale amejikuta yeye mwenyewe hana nafasi pale Madrid, huku fowadi huyo akicheza dakika 100 kwenye LaLiga tangu ligi hiyo iliporudi baada ya kusimama kwa miezi mitatu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mshindi huyo mara nne wa Ligi ya Mabingwa Ulaya alionekana kwenye kamera akiwa amevaa maski usoni mwake akiwa benchi kabla ya kucheka na wachezaji wenzake wakati Madrid wakiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Deportivo Alaves wiki iliyopita.

Bale alikuwa kwenye orodha ya wachezaji wa akiba wakati Madrid wakiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Granada na baadaye akiwa jukwaani alikuwa akitazama mchezo huo kwa kutumia darubini ndogo, na mchezaji mwenzake wa Tottenham, Berbatov amemshutumu mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales kwa tabia yake.

"Gareth Bale mara kwa mara anabeba vivywa vya habari kwa kujifanya amelala jukwaani wakati alipojua kwamba hatatumika licha ya kuwa kwenye orodha ya wachezaji wa akiba dhidi ya Granada," alisema Berbatov akiiambia Betfair.

"Wakati nilipoona vile, sikuamini. Nilimwona akivaa maski usoni na kujifanya amelala. Siwezi kumuunga mkono kwa hili. Ni tabia mbaya na kutokuwa na heshima kwa Real Madrid.

## HABARI MICHEZO

# PSG YAMTAKA DEMBELE, FEDHA KUMWACHIA NEYMAR




**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain imeripotiwa imeiambia Barcelona nini wanachokitaka kwa ajili ya kumruhusu Neymar kuondoka.

PSG wanataka euro milioni 80 na Ousmane Dembele kutoka Barcelona ili kubadilishana na Neymar, kwa mujibu wa El Chiringuito.

Neymar ameendelea kuhusishwa na mpango wa kurudi kwa miamba hao wa LaLiga, miaka mitatu baada ya kuondoka PSG kwa ada iliyokweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222.

Na Barcelona sasa inajua wazi nini ambacho PSG wanakitaka kuhusu kumwachia fowadi huyo kurudi pale Katalunya.

Dembele amekuwa akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara tangu alipotua pale Barcelona akitokea Borussia Dortmund mwaka 2017.

Kama ilivyo kwa Neymar, Mfaransa huyo naye amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka hapo Nou Camp.



# Sare Sassuolo yamshangaza Sarri

**TURIN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Juventus, Maurizio Sarri, amepigwa na butwaa kwa timu yake kulazimishwa sare ya mabao 3-3 na Sassuolo, licha ya vinara hao wa Serie A kuongoza kwa muda mrefu.

Juve waliongoza kwa 2-0 dhidi ya Sassuolo, lakini wakajikuta wakishindwa kulinda uongozi wao ili kushinda taji lao la tisa mfululizo la Ligi Kuu Jumatano.

Juve ambao ni mabingwa watetezi – ambao waliongoza kwa 2-0 wakati walipofungwa 4-2 mbele ya AC Milan mapema mwezi huu, walianza kwa kuongoza kwa mabao mawili ndani ya dakika 12 kupitia kwa Danilo na Gonzalo Higuain kabla ya Filip Djuricic kupunguza moja kuelekea mapumziko.

Domenico Berardi akafunga la pili kwa mkwaju wa adhabu ndogo kabla ya kumtengenezea pande Francesco Caputo aliyefunga na kuwafanya Sassuolo kuwa mbele kwa 3-2 zikiwa zimesalia dakika tatu mpira kumalizika.

Alex Sandro aliwaokoa Juve kwa kusawazisha na kuwezesha kufikisha pointi 77 baada ya mechi 33 za ligi, wakiwazidi Atalanta pointi saba ambao wapo nafasi ya pili.

"Kocha alitarajia kiwango mwendelezo kwa timu yake, ni kitu ambacho tumekuwa tukikitafuta kwa muda. Tulikuwa na wakati mzuri sana, lakini nashindwa kuelewa nini kilichotokea," alisema Sarri akiiambia Sky Sport Italia.

"Nilishangazwa, kwamba tulikuwa mbele kwa 2-0, lakini baadaye sisi tukawa nyuma kwa 3-2, hakika nilipigwa na butwaa."

Juve itacheza na Lazio ambao wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo, Jumatatu jijini Turin.

# Klopp: Tumeshindwa kufikisha pointi 100

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesisitiza hajakosa furaha kuhusu Liverpool kushindwa kufikisha pointi 100 kwenye Ligi Kuu baada ya kufungwa na Arsenal.

Liverpool walichezea kichapo cha mabao 2-1 pale wenye dimba la Emirates Jumatano, na mabingwa hao wanaweza kupata pointi 99 msimu huu kama wakishinda mechi zote zilizobaki.

Lakini Klopp alisema kwake halikuwa jambo la kukatisha tamaa kwa kushindwa kupata pointi 100, rekodi iliyowekwa na Manchester City msimu wa 2017/18.

"Hapana, angalau bado, sijui kama zitakuja," alisema kocha huyo wa Liverpool akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini jambo la muhimu ni kwamba nataka tu pointi ambazo tunaweza kuzipata na tutaona nini kitakachotokea mwisho mwa msimu.


"Siwezi kuzungumzia kuhusu mtazamo hasi, kwa hakika kabisa nipo chanya kabisa, kuwa bingwa na kuwa na pointi 93 ni jambo la kujivunia pia.

"Kwa sababu kwa sasa hatuwezi tena kupata pointi 100 au mbili zaidi, maana huo ndio ukweli uliopo.

"Tunapata pointi tunazostahili na tutaona ni kiasi gani itakuwa. Wakati tuliopo tuna pointi 93, na tumebakiwa na mechi mbili, hizi ni mechi ngumu sio rahisi kama watu wanavyofikiria na vijana wapo tayari kwa hilo."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MAN UTD, POGBA WAFIKIA PAZURI

Kiungo huyo Mfaransa anatarajia kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na kumaliza...

**MANCHESTER,** England

INAELEZWA kuwa Paul Pogba anakaribia kukamilisha mchakato wa kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na Manchester United, ambao utamaliza uvumi kuhusiana na hatima yake uliokuwa unazungumzwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

**Kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa alijiandaa kuondoka United katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana, wakati klabu yake ya zamani ya Juventus na Real Madrid zikitajwa kumwania mshindi huyo wa Kombe la Dunia.**

Lakini baada ya kurejea akiwa fiti na kufanya kazi vema na Bruno Fernandes kwenye safu ya kiungo ya Ole Gunnar Solskjaer, nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 anatarajia kuongeza mkataba wa kubakia hapo Old Trafford, taarifa kamili kuhusiana na mkataba huo zitatangazwa ifikapo mwishoni mwa msimu, The Sun limeandika.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Kocha wa United, Solskjaer ameanza kumweka katika mipango yake ya baadaye kiungo huyo.

Wakati mkataba wa sasa wa Pogba unatarajiwa kumalizika mwakani, na United ina nafasi ya kumsainisha mkataba mwingine wa miezi 12, mkataba mpya utamfanya Mfaransa huyo akae klabuni hapo hadi mwaka 2025, hivyo kila upande, klabu na mchezaji husika atalazimika kutimiza majukumu yake.

Katika kikosi kilichofanya makosa na kumaliza mchezo na Southampton kwa sare ya mabao 2-2 Jumatatu usiku, Pogba ameendelea kuwa kwenye kiwango cha juu na United tangu kurejea kwa Ligi Kuu England hapo Juni 17, mwaka huu.

Baada ya kucheza mechi mbili tangu Septemba na kukaa nje kwa sababu ya kupata majereha ya mara kwa mara kabla ya corona, miezi mitatu ya ugonjwa huo ilimsaidia kiungo huyo aliyesajiliwa kwa dau la pauni milioni 89 kutoka Juventus mwaka 2016 kurejea uwanjani akiwa na makali.

Aliingia akitokea benchi na kufunga penalti ambayo iliwafanya watoke sare ya bao 1-1 dhidi ya Tottenham, alitoa pasi ya mwisho katika ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Brighton na alifunga katika mchezo mwingine walioshinda walipoikabili Aston Villa wiki iliyopita.

Inaonekana kucheza pamoja na Bruno Fernandes ambaye alisajiliwa katika dirisha dogo la Januari, kumemsaidia Pogba kurejea katika kiwango chake bora.

## ZISIKUPITE

### CITY YAMTAZAMA KOULIBALY

MANCHESTER City imewasilisha dau la pauni milioni 65 kwa Napoli ili kumpata Kalidou Koulibaly (29), anayetakiwa na Liverpool pamoja na Manchester United huku awali thamani yake pauni milioni 80. ***(Mirror)***

### MARTINEZ KUMRITHI AGUERO

MANCHESTER City imemtaja straika wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez (22), kuwa ndiye mrithi wa muda mrefu wa Sergio Aguero, ambaye sasa ana umri wa miaka 32. ***(Sky Sports)***

### HAVERTZ MAMBO BADO

BAYERN Munich inafikiria kumwondoa katika mipango yake kiungo wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz (21), ambaye anawindwa na Chelsea. ***(Sport Bild, via Mail)***

### ZAHA AGOMBEWA ULAYA

EVERTON, Atletico Madrid na Bayern Munich zinatarajiwa kuwasilisha ofa ya kumwania winga wa Crystal Palace na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha katika majira ya joto, huku pia Newcastle ikitajwa kumwinda mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Mail)***

### PICKFORD AKUMBUSHWA

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti amemweleza golikipa wa Timu ya Taifa ya England, Jordan Pickford (26), kuwa anatakiwa "kuimarisha kiwango chake". ***(Guardian)***

### BELLINGHAM KIMEELEWEKA

KIUNGO wa Birmingham, Jude Bellingham, 17, amekubali dau la pauni milioni 22.5 ili kujiunga na Borussia Dortmund ya Ujerumani. ***(Bild)***

### PARTEY AITOSA ARSENAL

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Partey (27), ameamua kukacha dili la kujiunga na Arsenal na kusaini mkataba mpya na Atletico Madrid, ambayo imemwongezea mshahara. ***(GhanaSoccerNet, via Mail)***

### LUIZ KUREJEA CITY

PEP Guardiola amefungua milango ya kumrejesha Mancheter City kiungo wa Aston Villa Mbrazili, Douglas Luiz (22), mara dirisha la usajili litakapofunguliwa hivi karibuni. ***(Birmingham Mail)***

### LALLANA ANUKIA LEICESTER

KIUNGO wa Liverpool, Adam Lallana (32), ambaye ataondoka katika kikosi cha mabingwa hao wa Ligi Kuu England akiwa mchezaji huru hivi karibuni, anawindwa na Leicester, Burnley na Brighton. ***(Star)***

### ROSE AIGANDA NEWCASTLE

BEKI wa Tottenham, Danny Rose anamatumaini mkataba wake wa mkopo katika kikosi cha Newcastle utabadilika na kuwa wa kudumu, wakati taarifa kutoka Italia zinasema nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 anatakiwa na Lazio. ***(Newcastle Chronicle)***

### UNITED KUMTUMIA DALOT

BEKI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Diogo Dalot (21), ambaye ameshindwa kupata namba katika mechi tisa zilizopita anatarajia kurejea kwenye kikosi cha Manchester United kama Luke Shaw na Brandon Williams watakosekana kwenye mechi ya jana dhidi ya Crystal Palace. ***(Manchester Evening News)***

## ZFF yapongezwa kuandaa mafunzo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUFUNZI wa makocha wa magolikipa wa kimataifa anayetambulika na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Saleh Machupa, amesema huu ni wakati sahihi kwa Shirikisho la Mchezo huo Zanzibar (ZFF), kuendesha kozi maalumu ya idara hiyo ili kukuza viwango vya wachezaji wao.

ZFF imeandaa kozi ya ngazi ya kati ya magolikipa kuanzia Agosti 10, mwaka huu na inatarajiwa kushirikisha makocha 35 kutoka ndani na nje ya Zanzibar.

Machupa aliliambia gazeti hili makocha waliokuwapo walikuwa wanafundisha kwa kutumia vipaji, lakini baada ya kozi hiyo kufanyika, watakuwa wanatoa mafunzo kwa kufuata misingi.

Mkufunzi huyo alisema kulingana na mahitaji halisi yaliyoko katika soka, umefika wakati makocha wakawa na taaluma rasmi ili kuongeza ufanisi kwenye majukumu yao.

"Hivi sasa ni muhimu kuwa na taaluma kuliko kipaji, ukiwa na elimu pamoja na kipaji basi utapata kazi sehemu yoyote kulingana na jitihada zako, hivyo mie nawasihi makocha waone umuhimu wa kufanya kozi mbalimbali pale zinapotokea," alisema Machupa.

Aliweka wazi changamoto ya kupoteza magolikipa bora imetokana na timu kutoona umuhimu wa kuwaajiri makocha wenye taaluma na hii itasaidia kuwajenga magolikipa wao wakati wanapokuwa langoni.

## Marsh yajipanga kuimaliza Mlandizi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Marsh Queens, Aaron George, amesema amejipanga kuhakikisha anapata ushindi katika michezo yake miwili watakayocheza nyumbani ikiwamo dhidi ya Mlandizi Queens kutoka Mlandizi, Pwani.

Marsh Queens inatarajiwa kuwakaribisha Mlandizi Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza.

George alisema baada ya kupoteza pointi tatu dhidi ya Simba Queens mapema wiki hii, sasa amejipanga kurekebisha makosa na kulipa kisasi kwa Mlandizi Queens.

Kocha huyo alisema tayari ameyafanyia kazi mapungufu aliyoyaona katika mechi iliyopita na anaamini wataingia uwanjani kusaka pointi tatu na hatimaye kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo.

"Tumepoteza mechi dhidi ya Simba (Queens), kwa kufungwa mabao matano, mabao hayo ni mengi sana kwetu, sasa hatutakuwa tayari kupoteza alama, hatutazembea tukiwa katika uwanja wa nyumbani," alisema George.

Kocha huyo alisema hawako katika nafasi nzuri na wanatakiwa kushinda mechi zilizobaki ili kujiondoa kwenye hatari ya kushuka daraja.

Marsh Queens ipo katika nafasi ya 11 ikiwa na pointi tisa wakati Panama Queens ya Iringa ndiyo inaburuza mkia.

# SINGIDA YACHEKELEA KUFUNGWA 'KIDUCHU'

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya timu yake kupoteza mchezo, Kocha Mkuu wa Singida United, Ramadhani Nswanzurwimo, amesema amefurahia kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake ambao walimaliza mechi dhidi ya Yanga kwa kupokea kichapo cha magoli 3-1.

**Nswanzurwimo alisema idadi hiyo ya mabao waliyofungwa na Yanga ni chache, ukilinganisha na vichapo walichopokea kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na Azam.**

Kocha huyo alisema vijana wake walicheza mpira mzuri na hawakucheza kama timu iliyoshuka daraja.

"Vijana walicheza vizuri mno. Hatukucheza kama timu ambayo imeshuka daraja, hiyo ni faraja sana. Niliangalia goli la tatu, ingawa sikuangalia vizuri sana, lakini ni kama mchezaji wa Yanga alikuwa ameotea," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Aliongeza matokeo ya mchezo huo wa juzi yanaonyesha wazi kwamba kikosi chake kimeanza kuimarika kwa kupunguza idadi ya magoli yanayotinga kwenye lango lao kutoka kwa klabu kubwa hapa nchini.

"Tulifungwa magoli 8-0 na Simba, tukafungwa mabao 7-0 na Azam, lakini kuanzia hapo tukaanza kupunguza makosa na kucheza mpira mzuri pamoja na kwamba tumefungwa, lakini siyo idadi kubwa ya magoli, pia tulifungwa mabao 3-2 na KMC, na Yanga tumefungwa 3-1, vijana wanaonekana wameimarika ingawa tayari tumeshashuka daraja," kocha huyo alisema .

Aliweka wazi hana uhakika wa kuendelea kubaki kwenye kikosi hicho, kama baadhi ya mambo hayatarekebishwa.

"Nimeifundisha timu hii kwenye mazingira magumu mno, ikiendelea hivi na kama uongozi haujakaa chini na kurekebisha matatizo, sidhani kama naweza kuendelea na timu hii." Alimaliza Mrundi huyo.




Wachezaji wa DTB (jezi nyekundu) wakikabiliana na wenzao wa Ukonga Kings katika mechi ya Ligi ya Kikapu ya RBA iliyochezwa jijini Dar es Salaam mapema mwaka huu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *DTB yang'ara Ligi ya kikapu Dar*

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Benki ya DTB imeonyesha umahiri katika Ligi ya Kikapu Mkoa wa Dar es Salaam inayoendelea msimu huu baada ya kupanda daraja.

Kabla ya kuahirishwa kwa Ligi ya RBA kufuatia mlipuko wa corona, DTB ilikuwa imeshinda michezo yote miwili mfululizo dhidi ya vijana wa Don Bosco Youngsters kwa matokeo ya vikapu 72-44 na iliipa kichapo cha vikapu 58-48 timu ya Ukonga Kings.

Baada ya kurejea kwa shughuli za michezo nchini mapema Julai, uongozi wa RBA ulikutana na wawakilishi wa vilabu vyote vinavyoshiriki katia ligi hiyo na kuamua kufuta matokeo yote ya awali na kukubaliana na mfumo wa kucheza mara kwa kila timu na timu zingine badala ya mfumo wa kucheza michezo miwili yaani nyumbani na ugenini.

"Tunahitaji kumaliza msimu wetu mapema Oktoba, ili kuruhusu wachezaji kushiriki katika Timu ya Taifa na kalenda ya Shirikisho la Mchezo wa Kipapu - TBF," alisema Katibu Mkuu wa RBA, Daniel Kapongo.

DTB imefanikiwa kuendeleza rekodi ya ushindi kwa asilimia 100 ndani ya Ligi ya RBA msimu huu kwa kuwafunga Oilers kwa vikapu 63-52, Chui vikapu 67-34 na kuwalaza Mabibo Bullets vikapu 66-59 na kuweka rekodi ya kipekee kwa timu inayoshiriki ligi hiyo.

Kikosi cha DTB kinaongozwa na wachezaji mahiri kama Alex Bwana, Cornelius Mgaza na Englebert Machumu ambao wote kwa pamoja wameweza kukusanya alama 122 katika michezo mitatu iliyochezwa baada ya kurejea kwa ligi. Wachezaji wengine katika timu hiyo ni Akram Abdulmajid, Boaz Nsagalufu na mkongwe Frank Mwemezi.

Pazi ndiye mpinzani mkuu wa DTB na watakutana katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Bandari.

"Hii itakuwa ni mechi ngumu kuliko zingine zote tulizocheza msimu huu. Hivi karibuni timu ya Pazi iliwatwanga mabingwa wa RBA mwaka jana - timu ya Vijana. Tumejiandaa kwa mechi kama hii, kikosi kiko sawa,kimejitayarisha kisaikolojia na tuko tayari kwa ajili ya mechi ya Jumamosi hii saa mbili usiku. Napenda kuwaalika mashabiki wote wa mpira wa kikapu Dar es Saalam kuja kushuhudia mpambano huu mkali dhiidi ya Pazi," alisema Leonard Haule, nahodha wa DTB.

# Michezo

Ijumaa Julai 17, 2020

Nipashe




United, Pogba wafikia pazuri UKURASA 22



Kiungo wa AFC Bournemouth, Jefferson Lerma (chini), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Manchester City, David Silva katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. City ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yatamba haiachi kitu

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU ikibakia na mechi tatu ili kumaliza msimu huu wa 2019/20 wa Ligi Kuu Tanzania Bara, mabingwa wa ligi hiyo, Simba wamesema wataendelea kujiimarisha ili kuchukua kikombe cha mashindano ya Kombe la FA.

Simba itavaana na Namungo FC katika mechi ya fainali ya Kombe la FA, itakayochezwa Agosti 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga mkoani, Rukwa.



Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola (pichani), aliliambia gazeti hili wanahitaji kukamilisha msimu kwa kutwaa kikombe na hawataingia uwanjani kuikabili Namungo kinyonge. Matola alisema kila mchezaji wa Simba amejiandaa kuonyesha kiwango cha juu katika mchezo huo ambao utawapa furaha mashabiki wao.

"Tunajua hakuna mechi rahisi, kila mechi kwetu ni sawa na fainali, na huko Rukwa tutakwenda katika kukamilisha msimu, tunajipanga kumaliza msimu kama tulivyouanza, lakini tunatakiwa kushinda mechi za ligi zilizobakia," alisema Matola.

Simba ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa tatu mfululizo, ilianza msimu huu kwa kunyakua Ngao ya Jamii kwa kuifunga Azam FC mabao 3-2.

# Yanga bado yaweweseka

**Na Saada Akida**

## Kocha wake Mbelgiji afunguka kichapo dhidi ya watani zao, Simba pia imewakosesha...

LICHA ya kupata ushindi mabao 3-1 dhidi ya Singida United na kujiimarisha katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema kichapo alichopokea kutoka kwa watani zao na kutolewa kwenye michuano ya Kombe la FA, bado kinamtesa.

**Yanga ilifungwa mabao 4-1 na kuondolewa kwenye mashindano ya Kombe la FA, na hivyo kupoteza tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), msimu ujao.**

Akizungumza na gazeti hili, Eymael alisema matokeo ya mchezo wa FA yanaendelea kumuumiza kwa sababu wameshindwa kutimiza malengo waliyokuwa nayo baada ya awali kushindwa kuchukua taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Eymael alisema mbali na kukosa tiketi ya kushiriki michuano ya CAF, timu yake pia imepoteza fedha ambazo wangepata baada ya kuifunga Simba na kuchukua kombe hilo.

Mbelgiji huyo alisema anahitaji kuendelea kurekebisha mapungufu ya kikosi chake ili wapate ushindi katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobakia na hatimaye kumaliza msimu kwa heshima.

"Timu imecheza vizuri na kupata ushindi, lakini bado nafasi ya ulinzi haijaimarika, natakiwa kufanyia kazi kwa sababu ukiangalia mechi unaona mabeki wanaruhusu mabao, kama leo (juzi) dhidi ya Singida United, tumeruhusu wapinzani wetu kupata bao," alisema Eymael.

Kocha huyo alisema matokeo dhidi ya Singida United yamewarejesha katika nafasi ya pili, lakini bado matokeo ya mchezo wao na Simba hawezi kuyasahau kutokana na kuwaondoa kwenye malengo.

"Ushindi huo ni sawa, ila tulitakiwa kupambana katika mchezo dhidi ya Simba, tumepoteza nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa pamoja na fedha ambazo tungepata katika FA, tunateseka," alisema kocha huyo.

Hata hivyo aliwapongeza nyota wake kwa kucheza vizuri katika mchezo huo wa juzi ingawa bado safu ya ulinzi inaendelea kuruhusu mabao kila wanaposhuka dimbani.

Naye Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, Hersi Said, amewataka mashabiki wa klabu hiyo kutulia na kushikamana ili dhamira ya kuboresha timu yao kwa ajili ya msimu ujao ikamilike.

Said alisema wamepoteza mechi yao dhidi ya Simba, lakini maisha mengine lazima yaendelee kwa sababu kwenye soka kuna kupata na kukosa.

"Kwetu matokeo ya mechi dhidi ya Simba yamepita, kwa sasa tunaendelea kujipanga kuhakikisha kikosi kinakuwa imara na bora kwa ajili ya msimu ujao, tunawaahidi msimu ujao hawataambulia chochote," Said alisema.

Aliahidi GSM itahakikisha mchakato wa usajili unafanyika kwa umakini na kiwango cha juu kwa kutekeleza mapendekezo yatakayotolewa na benchi la ufundi la timu hiyo.

"Kipigo cha Simba ni kikubwa, kwa matokeo yale tumepata nafasi ya kujifunza, tushikamane na wote tuwe na dhamira ya pamoja kuboresha timu yetu kwa ajili ya msimu ujao, tusonge mbele na yale ya Simba yamepita," Said alisisitiza.

Baada ya Yanga kutolewa kwenye michuano hiyo ya FA, sasa Namungo FC ya Lindi ambayo imetinga fainali, imepata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika huku Mabingwa wa Ligi Kuu, Simba wakienda kupeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >